# Nipashe

Jumamosi Septemba 7, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581792

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




UKURASA 22

**CASEMIRO AKATAA KUTUA GALATASARAY**

UKURASA 3

**Mongella** asema utekelezaji Ilani kwa vitendo ni mtaji ushindi CCM



UKURASA 4

**ACT** Wazalendo yatangaza Baraza la Mawaziri kivuli

UKURASA 5

**Mama,** mwanawe wauawa kinyama usiku na watu wasiojulikana

# AJALI TENA

• **Watu** 12 wafariki dunia na 36 kujeruhiwa, ni ya pili ndani ya wiki moja Mbeya...

*Endelea Ukurasa 2*



Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani, wakikagua mabaki ya basi la kampuni ya AN CLASSIC, lililopata ajali katika Kijiji cha Lwanjilo, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na kusababisha vifo vya watu 12 na kujeruhi 36. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Mbowe amgeuzia kibao Msigwa, ataka amlipe bil. 5/- madai ya kumkashifu

UK. 2



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akizungumza na wawekezaji na viongozi wa kampuni mbalimbali za China, jijini Beijing jana. Rais yuko nchini China kwa ziara ya kikazi ambapo alishiriki katika Mkutano wa Jukwaa la Ushirikiano kati ya China na Afrika (FOCAC). **PICHA: IKULU**

## Waziri Mkuu aibana wizara huduma za SGR

UKURASA 3

**MICHEZO** **YANGA : TUTAWAMALIZA CBE KWAO** UK.24

**MAONI,** UK.6

HABARI KITAIFA

## Mbowe amgeuzia kibao Msigwa, ataka amlipe fidia bil. 5/- madai kumkashfu

**Na Grace Gurisha**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amemtaka aliyekuwa mwanachama wa chama hicho, Peter Msigwa, kumlipa fidia ya Sh. bilioni tano ndani ya siku tano na kumwomba radhi.

Aidha, amesema iwapo Msigwa akishindwa kufanya hivyo atamburuza mahakamani Jumanne ijayo.

Pia Msigwa anatakiwa ndani ya siku hizo awe amemwomba radhi Mbowe kupitia vyombo mbalimbali vya habari ikiwamo katika magazeti ambayo yanapatikana nchi nzima.

Taarifa hiyo ya mahitaji (demand notice) imetolewa na jopo la mawakili wa Mbowe, Hekima Mwasipu, John Mallya, Simon Mrutu na Dickson Matata, kwa madai kwamba Msigwa amemchafua mteja wao.

Akizungumza jana kwa njia ya simu, Wakili Mwasipu alisema Msigwa anatakiwa kuyakamilisha hayo ndani ya siku tano tangu alipopokea taarifa hiyo, Septemba 4, mwaka huu.

"Anatakiwa kumlipa mteja wetu fidia ya Sh. bilioni tano pamoja na kumwomba msamaha hadharani kupitia vyombo vya habari, akishindwa kufanya hivi, Jumanne tunaingia mahakamani," alisema Wakili Mwasipu.

Wakili Mwasipu alisema fedha hizo ni kama adhabu maalum ya kuharibu taswira ya mteja wao kwa kumchafua.

Msigwa ambaye kwa sasa ni mwanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kupitia taarifa ya jopo hilo zimesema anatakiwa kufanya hivyo, kutokana na tuhuma za uongo alizozitoa dhidi ya Mbowe.

Inadaiwa kuwa taarifa hizo ziliharibu taswira yake ya kisiasa na kifamilia katika jamii na pia, inadaiwa katika taarifa hiyo Msigwa anamtuhumu Mbowe kuanzisha 'Mbowe Foundation' na kutumia helkopta kuzunguka nchini.

Taarifa hiyo imenukuu baadhi ya maneno ya Msigwa aliyoyatoa dhidi ya Mbowe kuwa: "Mheshimiwa Mbowe ana Foundation (taasisi) hiyo si siri anayo na hiyo Mbowe Foundation ndiyo 'actually' ina run (endesha) chama."



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera akiwajulia hali baadhi ya majeruhi wa ajali ya basi la AN CLASSIC, waliolazwa katika Kituo cha Afya Chalangwa, wilayani Chunya, jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Ajali yaua 12 na kujeruhi 36

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU 12 wamefariki dunia na wengine 36 kujeruhiwa baada ya basi walilokuwa wakitumia kusafiria kutoka Mbeya kwenda Tabora kuacha njia na kugonga gema kisha kupinduka.

Hiyo ni ajali ya pili ndani ya wiki moja baada ya ile iliyotokea mwanzoni mwa wiki wilayani Mbarali na kusababisha vifo vya watu tisa. Kwa ujumla, ajali hizo mbili zimeua zaidi ya watu 20 mkoani Mbeya ndani ya wiki moja.

Ajali hiyo ambayo ilitokea jana asubuhi katika kijiji cha Lwanjilo, wilayani Mbeya, ilihusisha basi la kampuni ya AN CLASSIC lenye namba za Usajili T 282 CXT.

Wakati ajali hiyo ikitokea, inadaiwa basi hilo lilikuwa na abiria kati ya 50 na 60 na kidhibiti mwendo kilikuwa kimezimwa kwa zaidi ya mwezi mmoja.

Baadhi ya mashuhuda wa ajali hiyo ambao walishiriki katika uokoaji, walisema basi hilo lilikuwa katika mwendokasi hali iliyosababisha dereva ashindwe kulimudu eneo hilo ambalo lina kona kali.

Balozi wa Kitongoji cha Nsalaga mahali ilipotokea ajali hiyo, Isaka Mbuba, alisema alishuhudia basi hilo likianguka wakati alipokuwa katika harakati za kuwatangazia wananchi wake kuhudhuria mkutano wa kitongoji.

Alisema aliliona gari hilo likiwa kwenye mwendokasi wakati anasalimiana na mmoja wa wananchi wake na muda mfupi akasikia kishindo na alipogeuka aliliona limepindua huku abiria wakipiga kelele za kuomba msaada.

Mbuba alisema aliposogea eneo la tukio alikuta watu wengi wameumia na wengine wakiwa wameminywa na gari chini, ndipo alipompigia simu mwenyekiti wa kijiji kumjulisha.

Kaimu Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi (ACP) Wilbert Siwa, alisema chanzo cha ajali hiyo ni uzembe wa dereva wa basi hilo ambaye alikuwa anaendesha kwa mwendokasi.

Alisema dereva alishindwa kulimudu gari katika eneo hilo kutokana na kuwa na kona kali ambayo ilistahili apunguze mwendo na hivyo akaenda kugonga gema na kisha gari kupinduka.

Kamanda Siwa alisema baadhi ya abiria wamefariki dunia papo hapo na wengine walipatiwa matibabu katika Kituo cha Afya cha Chalangwa na Hospitali ya Wilaya ya Chunya.

"Bahati mbaya ni kwamba hata dereva mwenyewe amefariki dunia. baadhi ya miili imehifadhiwa katika Kituo cha Afya Chalangwa na mingine ipo hospitali ya wilaya," alisema.

Mmoja wa majeruhi waliolazwa katika Kituo cha Afya Chalangwa, Hamadi Mazinge, alisema alikuwa anatoka Mbeya kwenda nyumbani kwao, Lupa Tingatinga, wilayani Chunya.

Alisema tangu wakati wanatoka Mbeya, dereva alikuwa anaendesha kwa mwendokasi na kwamba kuna wakati walimtaka apunguze, lakini aliendelea kuendesha hivyo hadi buti kufunguka na mizigo kuanguka.

"Baada ya mizigo kuanguka alisimamisha gari na tukaipakia upya, wakati tunapakia mabasi mengine yalitupita ndipo dereva akatuambia tupande haraka tuondoke. Kwa hiyo alikuwa anakimbiza ili tuyakute mabasi yaliyokuwa yametupita.

Hatukuelewa kilichotokea tukajikuta tu tupo chini," alisema Mazinge.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ambaye alifika eneo la ajali, alisema baada ya uchunguzi walibaini kuwa kidhibiti mwendo cha basi hilo kilikuwa kimezimwa kwa zaidi ya mwezi mmoja.

Homera aliagiza Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa ardhini (LATRA) kufuatilia mabasi yote na kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wamiliki wa mabasi watakaobainika kuchezea mfumo wa vidhibiti mwendo hivyo.

Pia aliagiza Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) mkoani hapa kuweka vibao vya tahadhari katika maeneo yote ya miteremko na kona kali.

# Mongella asema utekelezaji wa ilani mtaji wa ushindi CCM

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, John Mongella, amesema baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Chama 2020-2024, amejiridhisha kwamba chama kinaingia katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu ujao kwa uhakika wa ushindi wa kishindo.

Akizungumza baada ya kupokea taarifa hiyo jana kutoka Ofisi ya Mkoa wa Shinyanga, Mongella alisema kutokana na utekelezaji mzuri wa ilani, chama hicho kina uhakika wa ushindi na kwamba waendelee na kasi ya kuleta maendeleo ili kero zote ziishe.

Mongella ambaye yuko kwenye ziara ya siku saba mkoani Shinyanga akiwa mlezi wa mkoa huo, pia aliwataka viongozi wa ngazi ya mkoa na hadi mitaa kufanya kazi ya kuwaletea maendeleo wananchi.

Alisema serikali chini ya Rais Samia suluhu Hassan imedhamiria kwa dhati kuboresha maisha ya wananchi ikiwa ni pamoja na kuleta pembejeo za kilimo kwa wakati, na maafisa ugani kutoa elimu kwa wakulima.

Awali, akizungumzia kilimo, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, alisema kutokana na mvua nyingi za msimu wa kilimo uliopita, uzalishaji wa pamba umepungua lakini mazao mengine kama tumbaku na mpunga ni wa kuridhisha.

Alisema kwa sasa serikali imejikita kuhakikisha miradi yote iliyoko kwenye ahadi za uchaguzi 2020-2025 inatekelezeka kwa wakati.

Pia Mongella alisisitiza umuhimu wa vijana kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo, akibainisha kuwa wao ni nguvu kazi ya taifa na wanayo nafasi kubwa ya kuchangia ustawi wa jamii.

Alisema ni muhimu kwa vijana kujihusisha na kilimo cha kisasa na kutumia teknolojia ili kuongeza tija. Naibu katibu Mkuu alipongeza juhudi za serikali katika kutekeleza miradi ya maendeleo, ikiwemo ujenzi wa barabara, hospitali, na shule, na kusema kuwa juhudi hizo zimeongeza imani ya wananchi kwa chama hicho.

Alisema serikali inatekeleza kwa vitendo ahadi zake na kwamba wananchi wanaona mabadiliko.

Kuhusu afya, Mongella alisifu serikali kwa kuboresha sekta hiyo ikiwamo kuongeza upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika vituo vya afya. Alisema hatua hiyo imepunguza vifo vya kinamama na watoto na kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa.

Vilevile, alitoa wito kwa viongozi wa afya kuongeza juhudi katika kutoa elimu ya afya kwa wananchi.

Alipongeza jitihada za viongozi wa mkoa katika kupambana na rushwa na ufisadi, akisema kuwa vitendo hivyo vinadhoofisha juhudi za maendeleo.

Mongella alisisitiza umuhimu wa kuwa na viongozi waadilifu na wenye kujali maslahi ya wananchi, na kuwaasa wananchi kuwafichua wale wote wanaojihusisha na vitendo vya rushwa.

Pia alizungumzia umuhimu wa mazingira na alitoa wito kwa wananchi wa Shinyanga kupanda miti na kulinda vyanzo vya maji.

Alisema suala la uhifadhi wa mazingira ni jukumu la kila mmoja, na kwamba serikali itaendelea kutoa ushirikiano ili kuhakikisha mazingira yanakuwa salama kwa kizazi cha sasa na kijacho.

Katika ziara yake, Mongella atatembelea Shinyanga Mjini, Kahama, Msalala, Ushetu, Shinyanga Vijijini na kufanya mikutano ya ndani na ya hadhara.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akitoa hotuba ya kuahirisha shughuli za mkutano wa 16 wa Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Majaliwa aibana wizara huduma SGR

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametoa maelekezo mahsusi kwa wizara za Uchukuzi na Kilimo, likiwamo la kulisimamia Shirika la Reli Tanzania (TRC) kuhakikisha huduma na miundombinu ya treni ya mwendokasi (SGR) inaboreshwa ili mradi udumu kwa muda mrefu.

Akitoa hoja ya kuahirisha Bunge jana, Majaliwa aliitaka wizara hiyo kuendelea kulisimamia kwa karibu shirika hilo na kuhakikisha huduma za treni hiyo zinaboreshwa na miundombinu inaimarishwa.

Alisema Desemba 31, 2023, Rais Samia Suluhu Hassan alielekeza kuanza uendeshaji wa reli ya SGR kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Dodoma ifikapo Julai, mwaka huu, na safari zimeanza kwa kipande hicho.

Alifafanua kuwa katika mwaka wa fedha 2024/25, serikali itaendeleza sekta ya uchukuzi kwa kusimamia sekta ya reli ikiwamo ujenzi wa SGR na uendeshaji wa treni ya kisasa ya abiria Dar es Salaam-Dodoma.

Alisema treni hiyo inaendelea kutoa huduma kwa wananchi na imechangia kuimarisha sekta ya usafirishaji.

Majaliwa pia aliiagiza Wizara ya Kilimo isimamie kwa ukaribu upatikanaji na usambazaji wa pembejeo za kilimo hususani mbolea, ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya msimu ujao wa kilimo na kwa kuzingatia jiografia za kanda za kilimo nchini.

Kadhalika, aliwataka maofisa ugani waendelee kutoa elimu kwa wakulima kuhusu matumizi ya teknolojia bora za uhifadhi wa mazao ya chakula na matumizi sahihi ya chakula hicho katika ngazi ya familia.

Kuhusu Rais Samia kuwa Rais Bora Afrika 2023, Majaliwa alisema ametajwa baada ya kuleta mabadiliko makubwa ambayo yameiinua Tanzania na kuing'arisha katika ukuaji wa uchumi, utawala bora na mageuzi ya kijamii.

Alisema Agosti 15, mwaka huu, Jarida la The African Times USA lilimtangaza Rais Samia kutokana na kuvutiwa na jitihada zake za kuleta mabadiliko hayo.

"Jitihada zake za kukuza umoja, demokrasia na uwezeshaji wa wananchi zimekuwa mfano wa kuigwa na viongozi mbalimbali barani Afrika," alisema.

Alisema Rais Samia ameendelea kujenga miundombinu muhimu na mikubwa ikiwamo ya reli, viwanja vya ndege, mitambo ya kuzalisha umeme na barabara.

# NGO zaonywa mahaba binafsi elimu mpigakura

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, ameyataka Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGO) yatakayopata kibali cha kutoa elimu ya mpigakura kwa ajili ya uchaguzi kuwa na uzalendo na kuzuia mahaba yao kwa vyama vya siasa.

Pia ameyataka kuwa waaminifu katika fedha wanazozipata kutoka kwa wafadhili kwa kuhakikisha zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa ya kuondoa kero zinazowakabili watanzania.

Dk. Biteko aliyasema hayo jana jijini hapa katika kilele cha Jukwaa la Mwaka la NGO 2024 sambamba na uzinduzi wa kampeni ya kukabiliana na utapiamlo inayotekelezwa na Shirika la World Vision.

Alisema mashirika hayo yanapaswa kutekeleza majukumu yao kwa weledi na uzalendo wa hali ya juu na kutoa elimu kwa kuonesha umuhimu wa kupiga kura na kujizuia kuweka mahaba binafsi ya vyama katika mchakato huo.

"Ninafahamu ziko NGO zimepewa nafasi ya kutoa elimu ya mpigakura na kufanya uangalizi wa mchakato unaoendelea wa uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura. Nitumie fursa hii kuwaomba mwendelee kutekeleza majukumu yenu kwa weledi na uzalendo wa hali ya juu, mtoe elimu ya mpigakura na kuchagua viongozi wanaofaa.

"Yawezekana kama binadamu mna mahaba na vyama vyenu, mna mapenzi na mtu fulani, jizuieni kuweka mahaba binafsi katika mchakato huu mkubwa.

"Nyie hamwezi kugeuka kuwa adui wa serikali kwa mchango wetu katika jamii na serikali itaendelea kuunga mkono juhudi zenu kuhakikisha mambo mnayoyafanya yanawanufaisha watanzania kwanza, kuwaondoa umaskini na kuboresha hali zao," alisema.

Aliyataka mashirika hayo yasikubali fedha au mtu kuwatoa katika maadili ya mtanzania na kuleta utamaduni mpya usio wao, bali kuheshimu ili watanzania waone ni sehemu yao.

Dk. Biteko pia alisema Wizara ya Fedha iko katika mchakato wa uandaaji wa mwongozo wa ushirikiano na asasi zisizo za kiserikali utakaotambua mchango wa wao hususan katika bajeti ya serikali ambao utatambulika na utaongezeka maradufu.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alisema katika mashirika hayo 1,368, imebainika Sh. trilioni 2.6 zilipokewa na Sh. trilioni 2.4 zimetumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Alisema sekta iliyoongoza kwa mwaka 2023 ilikuwa ni sekta ya afya, ikifuatiwa na uwezeshaji wa jamii kiuchumi na ulinzi wa jamii.

Waziri Gwajima alitaja sekta nyingine ni pamoja na uhifadhi wa mazingira, sekta ya elimu, kilimo, utawala bora, maji, masuala ya jinsia na haki za binadamu.




Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Camillus Wambura akimvisha cheo cha Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Dora Kiteleki, mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro jana, baada ya kupandishwa cheo na Rais na Amiri Jeshi Mkuu, Dk. Samia Suluhu Hassan. **PICHA: JESHI LA POLISI**

# ACT-Wazalendo yatangaza baraza la mawaziri kivuli

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha ACT-Wazalendo Zanzibar kimetangaza baraza la mawaziri kivuli na kuteua mawaziri na manaibu watakaoongoza baraza hilo lenye sekta 16.

Mwenyekiti wa chama hicho, Othman Masoud Othman, alitangaza baraza hilo jana na kueleza jukumu kubwa lililonalo ni kufuatilia utendaji wa serikali kisera, kisheria na kiutendaji.

Kadhalika alisema kuona namna gani sera, sheria, utendaji, uamuzi na usimamizi wa shughuli za serikali unaathiri maendeleo na muhstakabali wa nchi na wananchi katika uchumi, ustawi wa jamii, usalama wa raia, utengamano wa kijamii, haki, amani na utulivu wa nchi.

Othman ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais, alisema baraza hilo litafuatilia mambo hayo kwa kuzingatia maslahi ya wananchi, hasa katika matumizi ya madaraka, rasilimali na fursa za nchi ili kuona kwamba, malengo muhimu yaliyoelezwa na Katiba ya Zanzibar na Katiba ya chama hicho yanatimizwa kwa ukamilifu.

Alisema miongoni mwa mambo yatayopewa kipaumbele maalum katika kazi za baraza ni ubora wa sera za kiuchumi na fedha, ufanisi katika huduma za kijamii ikiwamo afya na elimu.

Mengine aliyataja ni haki za raia katika ardhi na upatikanaji wa haki zao katika vyombo vya umma na vya kutoa haki, mapambano dhidi ya ufisadi na utengamano wa kijamii, amani na utulivu.

"Hapa nitanabahishe kuwa kuundwa kwa naraza hili hakutaondoa utaratibu wa chama wa mikutano ya hadhara. Baraza litakuwa tu ziada ya juhudi za chama kuwa sauti ya wananchi," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema pamoja na kutangazwa kwa baraza hilo, kiongozi wa chama kwa kushauriana na viongozi wenzake, ataendelea kufuatilia utendaji wa baraza na kufanya marekebisho kadri inavyohitajika.

Akitaja uteuzi wa wizara hizo za kisekta 16, Othman alisema mawaziri wanawake ni mmoja na wanaume 15, manaibu waziri wanawake tisa na wanaume sita na linaongozwa na Mkuu wa Kiongozi ambaye ni, Ismail Jussa Ladhu.

Alisema Halmashauri Kuu ya Taifa ya chama iliamua viongozi katika pande zote mbili, kuanzisha baraza la wasemaji kisekta na halmashauri kuu.

Alisema iliamua hivyo baada ya kuona kwamba matokeo ya uchaguzi wa mwaka 2020 yaliirudisha nchi katika mfumo usio rasmi wa chama kimoja na hivyo kuondoa sauti za wananchi katika vyombo vya kutunga sheria vya nchi.

Mbali na kupaza sauti na kutoa mawazo mbadala, Othman alisema limekuwa chuo muhimu ya kuwajengea uzoefu wanasiasa chipukizi na hata wale wakongwe ambao hawakuwa na ujuzi wa kutosha katika uendeshaji na usimamzi wa shughuli za serikali.

Wizara zilizounda baraza hilo ni; Uchumi Dira na Maendeleo; Utumishi wa Umma na Maadili ya Uongozi; Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Mipango Miji; Biashara, Uwekezaji na Uwezeshaji Kiuchumi; Katiba na Sheria; na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Zingine ni Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati; Mafuta na Gesi Asilia; Mawasiliano na Usafirishaji; Utalii na Urithi wa Taifa; Elimu, Ubunifu na Stadi za Ufundi; Afya; Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; Maendeleo ya Jamii, Wanawake, Watoto na Makundi Maalum; na Wizara ya Vijana na Ajira.

Wakizungumza na waandishi wa habari, wateule wa baraza hilo kivuli walisema wataitumikia nafasi waliopewa kwa sababu kuna mapungufu makubwa katika mipango ya utekelezaji wa serikali.

Waziri Kivuli wa Fedha, Uchumi na Dira ya Maendeleo, Prof. Omar Fakihi, alisema dhana yake kubwa ni kuhakikisha wanaunganisha Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambayo inatekelezwa na serikali pamoja kuangalia mazuri ambayo yamo katika Ilani ya ACT-Wazalendo na utekelezaji wa ahadi zilizotolewa.

"Kumekuwa na kero kubwa katika sera za kodi, kwa mfano kuna kodi nyingi za serikali zimeongezwa na wananchi zinawakera kwa hivyo tunatekeleza kuangalia kero za wananchi pamoja na ahadi zilizotolewa na CCM ambazo utekelezaji wake haupo," alisema.

Naibu Waziri Kivuli wa Kilimo na Uvuvi, Makiye Juma Ali, alisema uwapo wao utasaidia kuibua kero katika jamii na kuwa sauti za watu wasio na sauti.

# Makalla ajigamba CCM kuheshimu taratibu, sheria

**Na Salome Kitomari,** LONGIDO

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla, amesema chama hicho kimeonesha kwa vitendo kuwa pamoja na kwamba kinaongoza dola, kinaheshimu taratibu na sheria za nchi.

Akizungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara eneo la Kilimahe, Kata ya Mundarara, Arusha, Makalla alisema awali alipanga kutembelea eneo la Mamlaka ya Hifadhi Eneo la Ngorongoro (NCAA), lakini walikatazwa na polisi kutokana na hali inayoendelea eneo hilo.

Kwa mujibu wa Makalla, lengo la ziara hiyo ya siku sita katika baadhi ya wilaya za Mkoa wa Arusha na Manyara ni kuhusu uhai wa chama, maandalizi ya uchaguzi wa serikali za mitaa, kuangalia utekelezaji wa ilani na kusikiliza kero za wananchi.

Akiwa katika kikao na viongozi wa CCM wilaya na mkoa, alimpigia Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, ambaye aliahidi kufanya ziara wilayani humo, kutatua kero ya muda mrefu ya maji.

"Katika mikoa 17 tuliyopita, CCM ni imara kuliko wakati wowote, idadi ya wanachama inaongezeka kila siku, viongozi na wanachama wa upinzani wanarejea CCM. Hii inathibitisha CCM ni imara, ndio kimbilio la wote, tumeridhika kwamba chama kipo vizuri na mabalozi wetu wapo vizuri sana," alisema.

Makalla alisema uimara wa CCM ndio amani ya nchi na kwamba wataendelea kusimamia serikali na kuimarisha chama ili kuhakikisha amani na utulivu vinaendelea.

Alisema mwaka huu wa uchaguzi ni muhimu kwa maendeleo na kwamba shule, zahanati, madarasa na vituo vya afya vinajengwa maeneo ya vitongoji na vijiji.

"Ukishajiandikisha tunakuwa na uhakika kwamba, mko tayari kuipigia kura CCM. Tunawaomba Oktoba 11 hadi 20, mwaka huu, mjitokeze kwa wingi ili Novemba 27, mwaka huu, mkipe ushindi chama chetu," alisema.

Kwa mujibu wa Makalla, wanatambua kuna wenyeviti ni kero, wamewachoka, hivyo wawe na imani na CCM itawaletea wagombea safi wasio na kashfa au makandokando.

"Hatutawaletea anayeongoza migogoro katika vijiji, mbabe ambaye hataki kusoma taarifa ya mapato na matumizi. Mwenyekiti wa CCM Wilaya na Halmashauri Kuu yako tunawapa kazi hiyo tuleeteni waliosahihi,"alisema

"Muda wa kampeni vitapita vyama vya siasa vitasema fitina na majungu, wasikilizeni ila waambieni tunaelewa changamoto zetu maji, barabara na maeneo ya malisho ila waambieni yote mtayapata kupitia CCM," alisema.

Makalla alisema wapinzani hawana hoja bali wanadakia mambo yanatojitokeza nyakati husika, hivyo wasisahau kuwa Ilani ya CCM imetekelezwa vizuri ila matatizo hayawezi kuisha na kwamba hata nyumbani mtu hawezi kuzimaliza zote.

"Kuna watu wanataka kuwaaminisha kuwa nchi hii inawezekana kusiwe na changamoto yoyote, wakisema hivyo wake zao wako nje ya nchi. Ninawahidi kuwa changamoto zilizoko tunazijua na tutazitatua sisi Chama Cha Mapinduzi," alisema.

Makalla alisema amekuwa Mkuu wa Mkoa wa mikoa mitano na kwamba rekodi yake haijavunjwa hadi sasa na amekuwa Naibu Waziri wa Michezo na Naibu Waziri wa Maji, hivyo anazijua vyema shida za wananchi na anakuwa mastari wa mbele kuzitatua.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan amejenga shule ya kisasa kwa ajili ya wasichana hivyo, ni muhimu wakaitumia kwa watoto wao kupata elimu safi kwa manufaa yao.

Makalla aliwataka wananchi kutokubali kuchonganishwa na serikali kwa kuelezwa kwamba, kabila fulani halidhaminiwi na kusisitiza kuwa Tanzania ni moja na haina masuala ya makabila.

Alisema hofu inayosambazwa kwamba Rais Samia Suluhu Hassan anawahamisha wafugaji na kugawa maeneo yao ya malisho, si ya kweli bali ni siasa za uchonganishi.

"Tutaendelea kuhakikisha wafugaji wanakuwa katika maeneo yao, maeneo ya malisho yatatengwa, hivyo msikubali kudanganyika kwa kuwa CCM ina wajibu wa kuwaletea maendeleo na kutatua changamoto zao,"alisema Makalla.

Makalla alisema wamepokea kero 36 za wananchi na kwamba utaratibu wake ni kuandikisha kero na kuita wataalam wazisome na kupata ufumbuzi wa pamoja.

Miongoni mwa kero hizo alisema ni kuhusu barabara ya Longido-Mundarara, changamoto za kituo cha afya kutokana na watu wengi, watendaji wa vijiji ni pungufu, na wafugaji wana hofu ya kuhamishwa.

Nyingine alitaja ni viongozi wa jamii kunyimwa kufanya mikutano na Mkuu wa Wilaya aliyepita, mradi wa maji unaosuasua, ujenzi wa barabara kiwango cha lami na visima kufunikwa na maji.

# Mbunge ahoji vijana kukosa kazi madai ya kukosa uzoefu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Viti maalum (CCM), Amina Ali Mzee, amehoji mpango wa serikali wa kupunguza wimbi la vijana wanaomaliza masomo na kukosa kazi kutokana na sharti la vigezo vya uzoefu wa miaka miwili na zaidi.

Akiuliza swali bungeni jana, Mbunge huyo alisema kupitia maboresho ya sera ya maendeleo ya vijana ni upi mkakati wa serikali kuongeza ajira kwa vijana.

Akijibu maswali hayo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Ridhiwani Kikwete, alisema ili kuwezesha vijana wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu kuwa na uzoefu wa kazi pamoja na sifa zingine za kuajiriwa ndani na nje ya nchi.

"Serikali inaendelea na programu mbalimbali za mafunzo ya uzoefu wa kazi (internship) na maboresho ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007 ambayo inahimiza uwepo wa mfumo endelevu wa kuwajengea vijana ujuzi na stadi muhimu za kuajirika," alisema.

Alitoa wito kwa wahitimu kutumia fursa mbalimbali zinazotolewa na serikali kupitia Programu za Elimu, Mafunzo na Uwezeshaji Kiuchumi, kwa kutoa mikopo na mitaji, fursa za ajira rasmi na zisizo rasmi katika miradi ya serikali inayopatikana katika wizara za kisekta na sekta binafsi.

Aliwaasa waajiri wote wa sekta ya umma na binafsi kuendelea kutoa nafasi kwa vijana wahitimu wapate mafunzo ya uzoefu wa kazi kwa uratibu wa kitengo cha huduma za ajira kinachosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Kadhalika, alisema kupitia maboresho ya sera ya vijana miongoni mwa mambo yatakayofanyika ni kutambua vijana ni kina nani.

Alisema ndani ya sera moja ya kitu kikubwa kilichoongezwa ni kuhakikisha kunakuwepo na programu za malezi, ili kuwaandaa vijana kuweza kujiajiri wenyewe na si kusubiri ajira za serikali pekee.



Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira (JET), Dk. Ellen Otaru akizungumza wakati wa mkutano na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari wilayani Bagamoyo jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mama na mwanawe wauawa kinyama na watu wasiojulikana

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAMA na mtoto wake wa kike, wameuawa baada ya kufanyiwa vitendo vya ukatili na watu wasiojulikana usiku wa kuamkia jana katika mtaa wa Muungano, Kata ya Mkonze, jijini hapa.

Waliouawa ni Mwamvita Mwakibasi (33) na binti yake Salma Ramadhani (13), mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Mkonze, Dodoma.

Akizungumza na waandishi wa habari eneo la tukio, dada wa marehemu, Pendo Mwakibasi, alisema alipigiwa simu na mama yao mzazi anayeishi jijini Mbeya, usiku wa kuamkia jana majira ya saa 8:00 kwamba mdogo wake amevamiwa nyumbani kwake.

"Alinipigia simu kwamba nenda ninasikia huko mdogo wako amevamiwa na hiyo simu alipigiwa na mjukuu wake ambaye anakaa hapa aliyelala chumba kingine ana miaka kama 14," alisema.

Alisema alipofika alimkuta mdogo wake huyo pamoja na mtoto wake wakiwa katika hali mbaya wakitokwa damu sehemu mbalimbali za miili wakiwa hawawezi kuzungumza.

"Nilikuta mmoja kitandani na mwingine yuko chini damu zimetapakaa kitandani mabongemabonge, nikasema kuna usalama kweli, nikaita majirani wakaja, tukamchukua na kumpeleka hospitalini," alisema.

Alisema wakati tukio hilo likifanyika mdogo wake alikuwa amelala kitandani na watoto wake wawili wa kike mmoja mdogo, ambaye aliamka usiku na kutaka kwenda msalani na alipojaribu kumwamsha mama yake ndipo alipoona damu zimetakapaa mwilini.

"Ikabidi amwamshe kaka yake aliyekuwa chumba kingine ndio kutafuta simu ya mama yake hakuiona, ikabidi ampigie bibi yake ambaye ndiyo namba ameishika kichwani, ambaye ndiye mama yangu aliyeko Mbeya na yeye akanipigia," alisema.

Alisema alimkuta mdogo wake akiwa amelala hajiwezi ametapaa damu sehemu mbalimbali za mwili wake na mtoto akiwa anakoroma aliita majirani na kuwapeleka hospitalini.

"Sijui nini kimemkuta katika hali hiyo na jana (juzi) saa 11:00 jioni nilikuwa na Mwamvita na saa 12:00 huyu binti Salma nilikuwa naye," alisema.

Mkuu wa Polisi Wilaya ya Dodoma, Daniel Dendarugaho, amewataka wananchi kuwa watulivu wakati wakiendelea kufanya uchunguzi wa tukio hilo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, George Katabazi, alipotafutwa alisema yupo nje ya kituo, lakini amelisikia na akifika ofisini atatoa taarifa.

Hivi karibuni, matukio ya mauaji katika mkoa wa Dodoma yamekuwa yakitokea mara kwa mara na ndani ya wiki hii kumeripotiwa tukio la baba kumnajisi mtoto wake wa miezi sita na kumsabishia kifo lililotokea katika mtaa wa Mbuyuni.

# Neema wakulima parachichi soko la China

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WAKULIMA wa parachichi nchini wanatarajia kupata mafanikio makubwa kiuchumi baada ya China, taifa la pili kwa kuwa na watu wengi duniani kuidhinisha kampuni za ndani kuuza zao hilo moja kwa moja kwenye soko lake.

Wizara ya Kilimo imeiarifu rasmi taasisi kilele ya tasnia ya mboga na matunda, bingwa wa sekta hiyo, Tanzania Horticultural Association (TAHA) kuwa China imefungua milango kwa parachichi zinazozalishwa Tanzania tangu Agosti 14, mwaka huu.

Jitihada za kufungua soko la China zilianza mwaka 2018 wakati TAHA ilipobaini ukubwa na thamani ya soko hilo na kuiandikia barua serikali kupitia Wizara ya kilimo kuiomba kufanya kila namna kupitia njia rasmi na za kidiplomasia kufungua soko hilo. "Tunaishukuru Wizara ya Kilimo kwa kuwa tulipokwenda kwao mwaka 2018, kuwataarifu kuhusu soko la China, walionesha nia na utayari wa kufanya kazi na sisi kuhakikisha kuwa tunalifikia soko hilo. Tunashukuru pia Shiririka la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) kwa ushiriki wao katika jitihada hizi," alisema Ofisa Mtendaji Mkuu wa TAHA, Dk. Jacqueline Mkindi.

Hivi karibuni, kabla ya soko la China kufunguliwa Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe alizungumza na wanachama wa TAHA kuwafahamisha kuwa serikali ilikuwa inafanya kazi kwa muda wa ziada kukamilisha taratibu rasmi za China kufungua soko la zao la parachichi.

Uamuzi huo wa China unatarajiwa kuwa neema kubwa kwa wakulima wa Tanzania na wauzaji zao hilo nje, kwa sababu China ina uhitaji mkubwa wa parachichi. Takwimu za Kituo cha Biashara la Kimataifa zinaonyesha China mwaka 2023 iliagiza tani 66,000 za parachichi zenye thamani ya dola za kimarekani milioni 151.

Kuongezeka kwa hamu ya Uchina ya parachichi, ambayo kwa kiasi kikubwa inasukumwa na watu wa tabaka la kati wanaojali afya zao, imebadilisha "tunda la siagi" ambalo halikuwahi kuwa maarufu hadi kuwa tunda lenye thamani kubwa katika soko la matunda nchini China.

Ingawa Tanzania ni nchi ya tatu kwa uzalishaji wa parachichi barani Afrika, baada ya Afrika Kusini na Kenya, wakulima wake hawakuwahi kusafirisha zao lao katika soko la China, kutokana na kukosekana kwa mkataba wa usafi na uhifadhi wa mimea (SPS). Ikiwa na idadi ya watu inayozidi bilioni 1.4, China kwa sasa ni nchi ya 10 kwa uagizaji wa parachichi duniani, na hivi karibuni inatarajiwa kuwa soko kuu la Tanzania la matunda hayo, ambayo tangu jadi yamekuwa yakiuzwa Ulaya na Mashariki ya Kati.

Wakati wa ziara ya kwanza ya Rais Samia Suluhu Hassan huko Beijing, Tanzania na China zilitia saini itifaki ya mahitaji ya usafi na uhifadhi wa mimea (SPS) ili kuwezesha parachichi zinazolimwa Tanzania kuingia katika soko kubwa la China.

Dk. Mkindi alieleza kufurahishwa kwake na kusema kuwa kitendo cha China kufungua soko lake kitaleta manufaa makubwa kwa wakulima wa ndani na kuimarisha uhusiano wa kibiashara kati ya mataifa rafiki hayo mawili.

Aidha alimpongeza Rais Samia kwa juhudi zake za kipekee za kidiplomasia, ambazo zilifikia kilele cha ufunguzi wa soko kubwa na lenye faida la China baada ya miaka sita ya jitihada zao kugonga mwamba.

Kwa mujibu wa Dk. Mkindi, mpango wa Rais kusaidia kufungua soko la China unaendana na mkakati wa kitaifa wa Tanzania wa kuongeza thamani ya mauzo ya nje ya horticulture hadi kufikia dola bilioni 2 kila mwaka,

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga, msiwadharau wapinzani michuano ya CAF

**WAKATI** Azam FC ikiwa bado inaugulia maumivu ya kuondolewa mapema katika mashindano ya kimataifa Ligi ya Mabingwa Afrika na APR kutoka Rwanda, Tanzania imebakia na wawakilishi wawili tu kwenye michuano ya kimataifa inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Mashindano hayo yanayosimamiwa pia na CAF, hufanyika kila mwaka na baadhi ya timu huanzia katika hatua ya awali, huku nyingine zikisubiri raundi ya kwanza, na hii hutokana na matokeo ya ushiriki wake.

Azam ambayo ilikaa miaka 10 bila kushiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, iliondolewa katika mashindano hayo baada ya kufungwa mabao 2-0 ugenini, kufuatia ushindi mwembamba wa bao 1-0 waliopata wakiwa nyumbani kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Kufuatia matokeo hayo mabaya, matajiri hao wa Chamazi walitangaza kuachana na kocha wao Msenegal Yousouph Dabo, na sasa wanajipanga kutangaza benchi la ufundi jipya.

Timu nyingine za Tanzania zilizoondolewa katika hatua ya awali ya mashindano hayo ya kimataifa ya CAF ni pamoja na Coastal Union ya jijini, Tanga, JKU na Uhamiaji zote za Zanzibar.

Ili kupata matokeo mazuri katika mashindano hayo, huanzia kwenye mchakato wa kusajili wachezaji wenye ubora ambao unafanana na ukubwa wa mashindano hayo ambayo mabingwa hujizolea zawadi nono ya fedha zinazotolewa na shirikisho hilo linalosimamia nchi wanachama 54.

Klabu inayofanya usajili kwa kufuata mapendekezo ya benchi la ufundi, ina nafasi kubwa ya kufanya vizuri katika mashindano yote itakayoshiriki huku ile ambayo bado inajiendesha 'kizamani' kwa viongozi kuchukua jukumu la kusimamia usajili.

Viongozi wa timu zilizofuzu kushiriki mashindano hayo ya CAF waache kujiendesha kwa mazoea, soka la sasa linahitaji kusimamiwa kwa kufuata misingi sahihi, kuendesha klabu kwa weledi husaidia na hurahisisha timu kufanya vizuri katika michuano yote itakayoshiriki.

Na itakapofika wakati wa dirisha dogo, ni muda wa viongozi kuliachia nafasi na kuwapa nguvu makocha kuamua wanahitaji wapi kuongeza nguvu ili kufikia malengo.

Klabu pia zinatakiwa kuwaandaa wachezaji kuheshimu wapinzani wao ndani na nje ya uwanja, wawaeleze wachezaji nidhamu bora husaidia kunyanyua viwango vyao kwa sababu wakati wote watakuwa wanafanya mambo ambayo hayaendi kinyume na mwongozo unaowahusu na kuipa timu matokeo chanya.

Tunawakumbusha Simba na Yanga kujiimarisha zaidi ili kuendelea kupeperusha vyema bendera ya Tanzania katika mashindano hayo.

Huu si wakati wa kumtathimini mpinzani kwa kuangalia jina lake na kujifananisha na jina la klabu yako, ikumbukwe katika soka lolote linaweza kutokea.

Makocha huu ni wakati wa kufanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika mechi zilizopita kwa sababu haitapondeza kuona timu hizo mbili zilizobakia pia zinashindwa kusonga mbele.

Ni wazi Yanga itaingia uwanjani kuwakabili mabingwa wa Ligi Kuu Ethiopia, CBE huku wakiwa na kumbukumbu ya ushindi mnono wa jumla wa mabao 10-0 waliyoyapata walipocheza dhidi ya Vital'O ya Burundi. Yanga inatakiwa ifahamu Septemba 13, mwaka huu itashuka dimbani kucheza na timu tofauti ambayo nayo imejipanga na inahitaji kupata matokeo bora iwe nyumbani au ugenini, kamwe isiingie ikiwadharau Wahabeshi hao, ijipange kupambana na kusahau ilichapata dhidi ya Warundi.


Pia tunawakumbusha Simba kujipamba imara kuhakikisha inapata matokeo mazuri ugenini Libya inapowafuata Al Ahly Tripoli na kurejea nyumbani kumalizia kibarua chao, kila mchezaji anatakiwa afahamu hakuna mechi rahisi na hakuna kinachoshindikana endapo juhudi zitaonekana ndani ya dakika 180.

Mungu ibariki Yanga, Mungu ibariki Simba katika kupeperusha bendera ya Tanzania kwenye michuano ya CAF.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Ni mapema sana kutupiana lawama, kuikatia tamaa Stars

**NI** mechi moja tu imechezwa na Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), dhidi ya Ethiopia, lakini ukisikia yale yanayozungumzwa na wadau na mashabiki wa soka, ni kama vile imeshindwa kufuzu kucheza fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON).

Sijajua ni kwa nini kelele zimekuwa nyingi kwa sababu ya kutoka suluhu tu, lakini binafsi nadhani Watanzania wengi walichukulia poa Ethiopia.

Waliona mapema ndiyo timu kibonde kuliko zote zilizopo katika Kundi H, na kudhani kila timu ikiwemo Tanzania kujichukulia kirahisi tu pointi sita kutoka kwao.

Bado mashabiki wengi wa soka nchini wanaishi kwenye zama za kujaji timu kutokana na jina lake, au nchi.

Walivyosikia Ethiopia basi akili ikawaambia ni timu dhaifu bila kujua, soka limebadilika sana duniani kwa sasa.

Hata huko Ulaya, baadhi ya nchi ambazo zilionekana zipo nyuma sana kimpira kwa sasa hazishikiki, zikizisumbua nchi ambazo zilikuwa wababe wa soka duniani.

Mfano mdogo tu hapa Afrika kuna nchi kama Comoro, Cape Verde, Mauritania, ni moja kati ya nchi zilizokuwa nyuma sana kisoka miaka ya 1970 hadi 1980, mpaka timu zao za klabu zilikuwa zikifungwa zaidi ya mabao 10 zinapocheza na timu za Tanzania, lakini leo hii wana kikosi bora cha timu ya taifa kinachotisha Afrika.

Hata Sudan Kusini, nchi iliyoundwa 2011 ambao bado tunawachukulia poa, wameshaanza kuamka, kama tusipoangalia kuna siku watakuja kutuvimbia tuje kushangaa. Mashabiki wa soka bado wanaendelea kukariri majina ya nchi ambazo kimpira zipo nyuma bila kujua kuwa wenzetu wanafanya mikakati ya muda mrefu kukuza soka lao, tena kwa njia mbalimbali ambazo wao wanaona zinafaa.

> **Hata huko Ulaya, baadhi ya nchi ambazo zilionekana zipo nyuma sana kimpira kwa sasa hazishikiki, zikizisumbua nchi ambazo zilikuwa wababe wa soka duniani.**

Wanazalisha wachezaji bora, wanapeleka vijana nje ya nchi, zipo hata nchi ambazo zinatumia uraia pacha, ukija kukutana nao baada ya miaka mitano ukadhani zipo vile vile unaumbuka.

Wakati tukidhani Ethiopia ni vibonde, rekodi zinaonyesha Stars imekutana na timu hiyo mara nne, mara tatu zilitoka sare na moja Tanzania ikipoteza.

Kwa maana hiyo Stars haijawahi kuifunga Ethiopia mechi yoyote rasmi ya kimashindano tangu mwaka 2013.

Sasa sidhani kelele hizi zinatoka wapi, wakati ule ulikuwa ni mpira ni mecho wa kwanza tu wa kundi.

Baada ya suluhu hiyo ya Jumatano, sidhani kama kuna haja ya kila mmoja kumtupia lawama mwenzake, maana naona mashabiki, wachambuzi wakiwa wanatupa lawama kwa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), makocha, wachezaji, ili mradi kila mmoja anakodhani ndiko kuna tatizo.

Badala yake tuchukulie kama ni matokeo ya kawaida kwani kuna michezo mingine mitano inakuja. Hakuna mahala palipoandikwa kuwa ni lazima tushinde nyumbani, badala yake tunatakiwa tufuzu bila kujali tutakaposhinda.

Ikumbukwe mara nyingi, Stars hufanya vyema zaidi ikicheza ugenini kuliko nyumbani, hivyo bado matumaini na makubwa ya kwenda Morocco mwakani yapo. Lakini hili litafanikishwa kwa kuendelea kuwa na watulivu na kuwapa viongozi, makocha na wachezaji ushirikiano badala ya kupiga kelele ambazo hazina msingi kwa sababu Stars haijapoteza mechi, imetoka sare tu.

# Uamuzi fidia mil. 300/- Septemba 11

Na Grace Gurisha

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam inatarajia kutoa uamuzi Septemba 11, mwaka huu, kama itaondoa mwenendo wa shauri la madai uliompa ushindi Leonard Kisena, kulipwa fidia ya Sh. milioni 300 au la.

Shauri hilo linatokana na basi la Kilimanjaro Express kusababisha kifo cha Immaculate Kisena (16), katika ajali iliyotokea Desemba 24, 2021.

Kisena ambaye ni baba wa marehemu Immaculate, katika tarehe hiyo akiwa na watoto wake wawili na mke wake, walikuwa safarini kwenda mkoani Kilimanjaro kwa ajili ya kusherehekea sikukuu za Krismas na Mwaka Mpya.

Inadaiwa walipofika eneo la Kamala, Bagamoyo saa 10:15 alfajiri, basi hilo liliacha njia na kuwagonga, hivyo kusababisha kifo cha Immaculate papo hapo. Immaculate alikuwa mwanafunzi wa kidato cha tano.

Ilidaiwa kuwa basi lililosababisha ajali hiyo ni lenye namba za usajili T 278 ALQ aina ya Scania na halikuwa na bima.

Mahakama hiyo ilifikia uamuzi wa kupanga tarehe hiyo baada ya kusikiliza maombi yaliyowasilishwa mahakamani hapo na mawakili wa Kampuni ya Kilimanjaro Truck Ltd na mapingamizi yaliyowasilishwa na Kisena kupinga maombi hayo ya kutaka shauri hilo lianze upya.

Jaji Wilfred Dyansobera aliwashukuru mawakili wa pande zote mbili kwa hoja walizoziwasilisha mbele yake na kupanga Septemba 11, mwaka huu, kutoa uamuzi huo wa maombi na pingamizi.

Tayari basi la Kilimanjaro lenye namba za usajili T 178 EAU liko mikononi mwa dalali wa mahakama, Daniel Mbuga wa kampuni ya Legit Auction Mart na linatarajiwa kupigwa mnada Septemba 13, mwaka huu.

Wakati wakiwasilisha hoja za maombi hayo, Wakili wa kampuni hiyo, Dickison Ngowi, aliomba mahakama kutupilia mbali uamuzi wake ambao kwa sasa uko katika utekelezaji.

Alidai kuwa kigezo ni kuwa katika uendeshaji wa shauri hilo, kuna taratibu za kisheria zilikosewa na kuiomba mahakama shauri hilo lianze upya.

Akijibu hoja hiyo, Wakili wa Kisena, Dk. Aloys Rugazia, akisaidiana na Valentine Charles, katika shauri la madai namba 47/2022, alidai kuwa makosa ya kimwenendo hayawezi kukosolewa katika mahakama hiyo iliyofanya uamuzi.

Alidai kuwa badala yake waleta maombi walipaswa kukata rufani kwa mujibu wa Sheria ya Madai (CPC), Kifungu cha 70 (2), lakini pia maombi hayo yaliwasilishwa mahakamani nje ya muda.

Jaji Dyansobera alisema maombi hayo yaliletwa chini ya hati ya dharura kwa hiyo pingamizi na maombi ya msingi yatasikilizwa kwa pamoja, ambapo ndicho kilichofanyika.

**NJE YA MAHAKAMA**

Kisena alisema safari ya kupigania utu na haki ya mwanawe marehemu Immaculate sio rahisi kwa kuwa kampuni hiyo ina uwezo wa kifedha, tangu mahakama ilivyoamua alipwe fidia wamekuwa wakiwasilisha pingamizi wakati hata katika usuluhishi hawakuwapo.

Wadaiwa katika shauri hilo namba 47,2022 ni Kampuni ya Kilimanjaro Truck Ltd, Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Roland Sawaya na Mjahidi Mohamed aliyekuwa dereva wa basi lililosababisha ajali lenye namba za usajili T 278 ALQ aina ya Scania

Kisena alifungua kesi hiyo, baada ya kupata ushindi katika Mahakama ya Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani ambayo ilimtia hatiani Mjahidi katika kesi ya trafiki kwa kukiri kuendesha gari hilo bila kuwa na bima, kusababisha kifo, majeruhi Omenis Kabora na uharibifu wa gari aina ya Toyota Land cruiser lenye namba za usajili T 323 CWB.

# Mnada wa magari chakavu ya serikali kufanyika mikoa tisa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa mwezi huu Wizara ya Fedha itaratibu na kusimamia minada kwenye taasisi 54 ya uondoshaji wa vyombo vya moto chakavu 150 katika mikoa tisa nchini.

Mikoa hiyo ni Dar es Salaam, Mbeya, Arusha, Morogoro, Mtwara, Njombe, Lindi, Pwani na Dodoma.

Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Liwale (CCM), Zuberi Kuchauka.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kuyauza magari mabovu yaliyoko katika halmashauri na ofisi za serikali nchini.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Chande alisema kwa mujibu wa miongozo iliyoko ya ufutaji na uondoshaji wa mali chakavu, ikijumuisha vyombo vya moto katika halmashauri na taasisi za serikali, Wizara ya Fedha ina jukumu la kuhakiki na kutoa vibali vya ufutaji na uondoshaji wa mali chakavu.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2023/24, Wizara ya Fedha ilitoa jumla ya vibali vya kuondosha mali chakavu 160 katika halmashauri na ofisi za serikali.

"Kati ya vibali hivyo, kulikuwa na vibali vya magari chakavu 976 yenye thamani ya Sh. bilioni 2.4. Magari chakavu 223 yenye thamani ya Sh. bilioni 1.6 yaliondoshwa kwa njia ya mnada kwa taasisi 54," alisema.

Vilevile, alisema ufualitiaji na tathmini ya magari ya miradi ulifanyika na kubaini magari 339 yenye thamani ya Sh. milioni 479.5 kuwa ni chakavu na taratibu za uondoshaji wake zinaendelea.

"Kati ya Julai na Agosti, mwaka huu, vibali 70 vya uondoshaji wa magari chakavu vimetolewa kwa halmashauri na ofisi za serikali," alisema.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selamani Jafo (katikati), akizungumza wakati alipotembelea Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Jafo ataka CBE kufundisha biashara kielektroniki

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo, amekitaka Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), kuwekeza katika ufundishaji wa programu za biashara ya elektroniki zitakazowawezesha vijana kufanya biashara kimataifa.

Alitoa rai hiyo jana jijini Dar es Salaam, alipotembelea chuo hicho katika sehemu ya mwendelezo wa ziara yake ya kutembelea taasisi zilizo chini ya wizara yake na kutoa maagizo.

Alikitaka chuo hicho kuendelea kuwa wabunifu kwa kozi zao ili ziende na wakati na kuwawezesha vijana wanaohitimu waweze kumudu kufanya biashara kitaifa na kimataifa na hivyo kukuza uchumi wao na taifa kwa ujumla.

Pia alikitaka chuo kujikita katika kutoa mafunzo ya kuwajengea maarifa wananchi na watumishi mbalimbali kupitia programu za muda mfupi hali itakayowezesha kuongeza weledi na ufanisi kiutendaji.

Waziri Jafo alikitaka chuo hicho pia kutoa mafunzo ya vitendo zaidi badala ya nadharia ili kuwawezesha wahitimu wa chuo hicho kumudu kujiajiri na kuajiri wenzao mara baada ya kuhitimu.

Alisema serikali inaendelea kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na kufanya baishara hivyo chuo hicho kinapaswa kuwaanda wanafunzi kujitegemea wanapohitimu badala ya kuhangaika kutafuta ajira.

Dk. Jafo alikipongeza chuo hicho kwa juhudi wanazofanya kuongeza udahili na kupanua miundombinu ya chuo hicho hali ambayo imekiwezesha kuongeza idadi ya wanafunzi mwaka hadi mwaka.

Alisema pamoja na mafanikio makubwa ambayo chuo hicho kimeyapata tangu kuanzishwa kwake bado kinahitaji kuongeza nguvu na kushirikiana na vyuo vingine vya ndani na nje ya nchi ili kufanikisha ndoto za vijana wa Tanzania.

"Ulimwengu unabadilika kwa kasi na biashara ndiyo jambo la msingi kwa hiyo tusisitize biashara kwasababu tunataka vijana wetu wafanye biashara kimataifa tuachane na analojia. Lazima vijana wetu wawe na uwezo wa kufanya biashara kielektroniki kimataifa," alisema Waziri Jafo

Awali, Mkuu wa Chuo hicho, Profesa Edda Lwoga, aliishukuru serikali ya Tanzania na Zanzibar kwa kuendelea kukisaidia chuo kupata maeneo ya kujitanua na kujenga kampasi zake na kwamba mpaka sasa wamefanikiwa kuwa na kampasi Mwanza, Mbeya, Dar es Salaam na Dodoma. Alisema kwa sasa chuo kimeanza kutoa maafunzo ya uanagenzi ambapo mwanafunzi anasoma nusu darasani na muda mwingine anautumia sehemu ya kazi ili kumpa ujuzi utakaomsaidia kujiajiri anapomaliza masomo yake chuoni hapo.

Prof. Lwoga alisema kupitia mpango huo wanashirikiana na taasisi na kampuni mbalimbali ambazo zimekuwa zikiwapa fursa ya mafunzo kwa vitendo wanafunzi wa chuo hicho na kwamba matokeo ya program hiyo imeendelea kuwa na mafanikio makubwa.

Alisema chuo kimewajengea uwezo wa kibiashara wajasiriamali wapatao 1,500 kwa mwaka wa fedha 2023/24 na kwamba mpango ni kuwafikia wafanyabiashara wengi zaidi ili kuwapa elimu hiyo.

"Tumeshasaini mkataba wa makubaliano baina yetu na Shirika la Viwango Tanzania TBS, Wakala wa Vipimo WMA kuhusu kozi ya metrolojia na tumeshasaini mkataba na serikali mtandao (eGA) kwaajili ya kutoa mafunzo teknolojia ya dijitali," alisema.

# Waganga tiba asili kupambana na wapotoshaji

Na Pilly Kigome

WAGANGA watafiti 250 wa magonjwa sugu wa tiba asili kutoka Afrika wapo nchini kutoa tiba asili bure kwa mzimu wa Afrika ulioko Chalinze, mkoani Pwani, na kupanga mikakati kutokomeza waganga washirikina wanaopotosha jamii.

Mganga Mshauri wa Umoja wa Waganga Afrika Mashariki, Dk. Riziki Malela, aliyasema hayo wakati akizungumzia maadhimisho ya mwaka mmoja ambayo yamekutanisha waganga hao kwa siku tatu kuanzia jana, Chalinze, mkoani Pwani, kwa ajili ya kuboresha huduma za matibabu.

Waganga hao ni kutoka nchi za Nigeria, Rwanda, Burundi, Afrika Kusini, Ethiopia, Kenya, Uganda na Tanzania yenyewe.

Dk. Malela alisema mkusanyiko huo umekuja kutembelea mzimu wa Afrika waliouzindua mwaka jana ulioko Chalinze, ikiwa na pamoja kukutana na kubadilishana ujuzi wa kitabibu kwa waganga hao.

"Tunakwenda kuidhihirishia dunia kwamba tiba asili zipo na Tanzania, ndio waasisi wa tiba zote za asili zilizoko ulimwenguni kwa sasa.

"Tnawaasa watanzania wasidharau tiba asili na mizimu waachane na waganga wa kishirikina," alisema Malela.

Mwenyekiti Kitaifa Shirika la Waganga wa Mitishamba na Utafiti Kenya, Ali Suleiman, alisema wamekuja Tanzania kwa ajili kujifunza na kubadilishana ujuzi wa matibabu kutoka kwa wenzao.

Alisema miongoni mwa mambo ya kujifunza ni kazi zinazofanywa na mzimu kusaidia jamii katika tiba za mwanadamu.

Suleiman alisema mzimu huo umendaliwa kwa ajili ya kuwasaidia watabibu Afrika, kuwaongezea nguvu kwa ajili ya yale magonjwa ambayo ni sugu na mazito katika kuwasaidia kuwatibia wagonjwa ikiwamo na kufanya maombi kutokana na changamoto zinazowakumba katika kazi zao.

Alisema wameunda umoja huo ili kuwapa fursa kubadilishana mbinu na ujuzi na kupanua wigo wa tiba kwa kuwa inatupa fursa ya kubadilishana maarifa katika sekta ya kutibia.

"Tumekuja kupanga mikakati ya kutokomeza waganga washirikina wanaoipotosha jamii kuwa ni waganga kumbe ni wahalifu ikiwamo na kuielimisha jamii kurithisha tamaduni na kuamini tiba za asili,"

"Tunaomba serikali zote Afrika, zituunge mkono katika kuwabaini na kuwasaka waharifu hao wanaoimaliza jamii na kuipotosha kuwa wao ni waganga, kumbe ni waharifu na baadaye mataifa yanateketea kwa vitendo vya kihalifu" alisema.

Mganga wa tiba asili kutoka Urambo, Tabora, Masudi Mkali, alisema maadhimisho hayo ya mwaka mmoja ya mzimu wa Afrika, yanalenga kusaidia watanzania wenye changamoto mbalimbali za kiafya kuwatibu kupitia mzimu huo.

"Tutatoa huduma za kuwahudumia wagonjwa wote bure huku tukiwa na malengo kuwaaminisha watanzania na waafrika, kuona umuhimu wa kudumisha mila na desturi pamoja na kuwaaminisha matibabu ya mitishamba inaponya" alisema Mkali.



Mkuu wa Mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi, akizungumza katika mkutano wa hadhara wa wakazi wa Kata ya Nyatwali, wilayani Bunda jana, kuhusu hatua zilizofikiwa na serikali za malipo yao kabla ya kuhamishwa eneo hilo, kupisha Hifadhi ya Serengeti. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbaroni tuhuma za mauaji watu wawili

Na Said Hamdani, LINDI

JESHI la Polisi mkoani Lindi linawashikilia watu wanane akiwamo mwanamke kwa tuhuma za mauaji ya wakazi wawili wa Kijiji cha Kitomanga, wilayani hapa yaliyotokea Juni, mwaka huu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Kamishna msaidizi (ACP) John Imori, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema watuhumiwa hao ambao hakuwataja majina yao, wamekamatwa Jumanne ya wiki hii kupitia msako uliofanyika kuanzia mwezi uliopita.

Kamanda Imori alisema Julai 13, mwaka huu, katika Kijiji cha Kitomanga, Wilaya ya Lindi, watuhumiwa hao wanadaiwa kuwaua Mwidini Mohamedi (69) na mtoto wake, Ramadhani Mwidini (10) kisha miili yao kuitelekeza shamba la jirani yao.

"Baada ya kuwahoji watuhumiwa hawa wanane, watatu kati yao akiwamo mwanamke, tumewabaini ndio wahusika wa mauaji ya watu hao na watano ni washirika wa tukio hilo baada ya kuwakuta na mali mbalimbali za marehemu zikiwamo luninga, simu na vitu vingine,"alisema Kamanda Imori.

# Kunenge ataja siri maendeleo uchumi na uzalendo

Na Julieth Mkireri, KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, amesema maendeleo ya kiuchumi yanazidi kukua kutokana na kuwapo kwa dhana ya uzalendo.

Amesema vijana hasa wanaopitia mafunzo jeshini wanapaswa kuendeleza dhana hiyo ili kasi ya ukuaji wa uchumi nchini iendelee.

Kunenge aliyasema hayo juzi wakati akifungua mafunzo ya vijana kwa mujibu wa sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Kikosi cha Ruvu.

Alisema kamwe taifa haliwezi kuwa na vijana wanaolalamika mara kwa mara na kushindwa kutumia fursa zilizoko kwa kuleta mabadiliko ya kiuchumi.

"Nikiangalia hapa ninawaona vijana wanaokwenda kuzitumia fursa bila kulalamika. Vijana mkizingatia mafunzo mliyopata tegemeeni kuiona kesho iliyobora," alisema.

Kunenge aliwataka vijana hao ambao ni wahitimu wa kidato cha sita, kuwa wabunifu kwa kutumia fursa zilizoko ili kuwa na taifa lenye maendeleo ya kiuchumi.

Mwakilishi kutoka Makao Makuu ya Jeshi ambaye pia ni Mkurugenzi wa Ustawi wa Jamii, Brigedia Jenerali Solotina Nshushi, amewakumbusha vijana hao kujiepusha na vitendo vitakavyosababisha afya ya akili na mwili kuzorota.

Kamanda wa Kikosi cha Jeshi la Kujenga Taifa, Ruvu, Kanali Peter Mnyani, aliwataka wazazi na walezi kutoacha kuwapeleka watoto wenye mahitaji maalum jeshini, kwani nao wana haki kama ilivyo kwa wengine.

Kanali Mnyani alisema kikosi hicho kilikuwa na vijana wenye mahitaji maalum ambao wameshiriki mafunzo hayo, kulingana na uwezo wao na wamepewa nafasi kama wengine kuonesha vipaji vyao. Mwakilishi wa wazazi ambaye pia ni, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, Regina Bieda, alisema wazazi na walezi wanatakiwa kuondokana na dhana potofu kwamba vijana wanaohudhuria mafunzo jeshini wanakwenda kuteswa.

"Mwanangu ni kati ya ambao walikuwa hawataki kuja jeshini akiogopa mateso, niliongea na askari walikuja kumchukua nyumbani na kumleta kikosini, sasa amekuwa shuhuda mzuri akijilaumu kwanini alikuwa anakataa kutokana na mafunzo mazuri aliyopata," alisema.

Bieda alisema ushuhuda alionao kupitia mtoto wake, unatakiwa uwe funzo kwa wazazi wengine kwa kuhakikisha wanaopangiwa jeshini, wanakwenda ili mafunzo hayo yawasaidie katika maisha yao na kuachana na kutegemea kuajiriwa.





## Waganga waonywa ramli chonganishi

**Thobias Mwanakatwe,**
MKALAMA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mkalama mkoani Singida, imewaonya Waganga wa Tiba Asili kujiepusha na ramli chonganishi ambazo zimekuwa chanzo cha fitina, mivutano na kusababisha migogoro katika jamii na familia.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Said Kalima, alitoa onyo hilo juzi wakati wa kikao maalumu cha kupeana elimu namna ya kufanya shughuli za tiba asilia ambacho kiliandaliwa na Mratibu wa Tiba ya Asilia, Josephine Makanyaga kutoka ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya ya Mkalama.

"Ramli chonganishi msifanye, serikali imeweza kuwatambua na inatambua uwepo wa tiba asili lakini katika tiba asili iendeshwe kwa utaratibu na ndio maana tumewaita kuwapa mafunzo," alisema.

Kalima alisema hivi sasa kumekuwa na wimbi la watu kupotea,watoto kuuliwa au watu wenye ulemavu wa aina fulani kukatwa viungo na sababu zinazotolewa ni kwamba wanaosababisha hayo yote yatokee ni waganga wa kienyeji.

Alisema serikali imekuwa ikijiuliza waganga wa kienyeji wanaofanya mambo hayo lengo lao ni nini na ndio maana ili kazi ya utoaji wa huduma ya tiba asili ifanyike vizuri na kwa ufanisi inawaita kuwapa mafunzo wafahamu namna wanavyopaswa kutekeleza majukumu yao kwa uwazi.

Tumewaita hapa tuelekezane na kutambuana kwamba huyu mzee anatoa tiba asili katika eneo fulani na amepata vibali vyake na elimu ukifanya kitu hiki ni kibaya," alisema.

Katika hatua nyingine, Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, Moses Machali, aliwataka wakuu wa idara, watumishi wa afya, watendaji kata na vijiji pamoja na maofisa Tarafa wilayani Mkalama kutoa elimu kwa wananchi namna ya kujilinda na ugonjwa wa homa ya Nyani maarufu kama Mpox.

Alitoa wito huo juzi wakati wa kikao cha afya ya Msingi wilayani Mkalama kilichofanyika kwenye ukumbi uliopo ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mkalama.

Aidha, katika kuhakikisha wananchi wanajilinda na ugonjwa huo, Machali amepiga marufuku wananchi kusalimiana kwa kupeana mikono ili kujilinda na ugonjwa huo.

Awali akiwasilisha hali ya ugonjwa huo, Ofisa Afya Wilaya ya Mkalama, Dorice Damiani amesema kuwa ugonjwa huo unaambukizwa kwa njia mbalimbali ikiwemo kushikana mikono, kujamiana na mtu mwenye ugonjwa huo pamoja na kuchangiana nguo.

# Chanzo Watoto kuacha masomo bayana

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

ASILIMIA 12 ya wanafunzi wa shule za msingi nchini wanaacha masomo kutokana na kukosa chakula huku asilimia 30 wakikabiliwa na tatizo la utapiamlo, imeelezwa.

Mkurugenzi wa World Vision Tanzania, James Anditi, alibainisha hayo jana, wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye Jukwaa la Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NACONGO) linalofanyika mkoani hapa.

Anditi alisema kuna baadhi ya watoto katika shulembalimbali wamekuwa wakikosa masomo kutokana na kukosa chakula wakati wa vipindi vya masomo ya darasani.

Alisema takwimu zinaonesha kuwa takribani asilimia 12 ya wanafunzi wanaacha masomo kwa sababu hiyo.

Pia alisema utapiamlo bado ni tatizo kubwa, hivyo linapaswa kujadiliwa ndiyo maana shirika hilo kwa kushirikiana na serikali, limeamua kukutana ili kuhakikisha tatizo hilo linatokomezwa.

"Ndani ya miaka mitatu, kampeni ya kutokomeza utapiamlo itafanyika vizuri kwa kushirikiana na serikali ili kuhakikisha watoto wanakwenda shuleni na kupata lishe," alisema Anditi.

Kwa mujibu Anditi, kampeni hiyo ya kupinga utapiamlo kwa watoto inayojulikana kama Enough, inatarajiwa kuzinduliwa jijini Dodoma huku akisisitiza kuwa, inatarajiwa kutekelezwa kikamilifu katika maeneo mbalimbali.

Alisema kampeni hiyo itatatua tatizo la utapiamlo kwa watoto wadogo lakini kwa watoto wa umri wa balehe ambao nao wako katika tatizo la kukosa masomo kutokana na kukosa lishe.

**"Baadhi ya watoto hawaendi shule kwa sababu ya utapiamlo, wengine wanakwenda shule hawajala, hivyo wakifika shuleni wanakosa chakula na wanaporudi nyumbani..**

"Mtoto akiwa na utapiamlo hata matokeo yake shuleni hayawezi kuwa mazuri ndiyo maana tumeamua kufanya hivyo ili kulikwamua tatizo hili," alisema Anditi.

Mtaalamu wa chakula na lishe kutoka World Vision Tanzania, Elizabeth Ndaba, alisema kumekuwa na sera na miongozo mbalimbali inayoelekeza namna ya kupambana na utapiamlo.

Alisema kampeni hiyo imebuniwa kuongeza nguvu katika kupambana na utapiamlo kwa watoto suala ambalo serikali inalipiga vita kila siku.

Alisema suala la utapiamlo ni mtambuka ndiyo maana limeleta wadau ili kuweka nguvu za pamoja kupinga utapiamlo kwa watoto wadogo lakini pia kwa wale wenye tatizo la ukosefu wa chakula katika umri wa kubalehe.

"Baadhi ya watoto hawaendi shule kwa sababu ya utapiamlo, wengine wanakwenda shule hawajala, hivyo wakifika shuleni wanakosa chakula na wanaporudi nyumbani kunakuwa hakuna chakula cha kutosha. Hili ni tatizo kubwa kwa watoto tunataka tuliondoe," alisema Ndaba.

Mwenyekiti wa Baraza la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Jasper Makala, alisema serikali imeweka vipaumbele ili kupunguza utapiamlo katika nchi.

Alisema vipaumbele hivyo vitafanyiwa kazi kwa ufasaha ili kuhakikisha mikakati waliyoipanga kama serikali na mashirika hayo kwenye kutatua tatizo la utapiamlo vinafanikiwa.




Baadhi ya wanafunzi wakipata maelezo walipotembelea banda la shirika la Akili Platform Tanzania (APT) katika maonesho ya shughuli mbalimbali za jukwaa la mashirika yasiyo ya kiserikali, jijini Dodoma, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Apigia debe malezi bora kwa watoto

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MWENYEKITI wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere (MNF) Mkoa wa Singida, Rajabu Mussa, amewataka wazazi, walezi na walimu kushirikiana kuimarisha malezi na maadili mema kwa Watoto.

Kwa kufanya hivyo, amesema kutajenga jamii nzuri ambayo itasaidia nchi katika kuleta maendeleo. Akizungumza jana wakati wa mahafali katika Shule ya Msingi Nkwe iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Singida, alisema kama watoto hawatatengenezewa mazingira mazuri wataingia mitaani na kujiingiza katika makundi mabaya ya wavuta bangi.

"Ndugu zangu wazazi, leo hii tuna majanga makubwa sana wananchi wa Nkwae, hivyo ni lazima tutambue kuwa watoto ni rasirimali kubwa sana kwani ndio kizazi ambacho kinakuja kuishika jamii baada ya sisi kuondoka," alisema.

Mussa alisema maadili na tabia njema huchangia kwa kiasi kikubwa katika kujenga na kuimarisha jamii yenye amani na umoja ambapo mtoto anapolelewa katika misingi ya maadili mema na tabia njema, inaimarisha uelewa na uwezo wake wa kupambanua matendo mema na mabaya.

Aliongeza kuwa wazazi pia wanajukumu la kuhakikisha watoto wao wanasoma kwani taifa ili liweze kuendelea ni lazima watu wasome ndipo maendeleo yatapatikana. "Wako watoto wanaona kutafuta pesa ni bora kuliko kusoma bila kujua kwamba taifa lolote ili liweze kupata maendeleo kila kijiji na kila mtaa lazima watu wasome ndipo maendeleo yapatikane," alisema.

Mussa alisema kijiji kama hakitakuwa na wasomi au taifa lolote au kijiji ambalo halitakuwa na wasomi litakuwa limekufa kwani ni jambo la wazi kwamba maendeleo yanaletwa na wasomi.

Mwenyekiti huyo alitahadharisha kipindi hiki wazazi kuwa makini na watoto wao kutokana na uwepo wa matukio ya ulawiti na ubakaji ambayo yameshika kasi kwa kuhakikisha wanachunguza watoto wao wanapokwenda na kurudi kutoka shule.

Kuhusu shule hiyo kukosa umeme, aliwaahidi kuwa yeye kwa kushirikiana na viongozi wa kijiji watawasiliana na Mkuu wa Wilaya kumjulisha changamoto hiyo ili umeme ufikishwe katika shule hiyo na hivyo kuwawezesha wanafunzi kusoma muda wote.





# Wizara na ZEEA kuinua wanawake wajasiriamali Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto imeahidi kuendelea kushirikiana na Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (ZEEA) katika kuwapatia wananchi fursa zitakazowasaidia kujikwamua kimaisha.

Fursa hizo pia zinalenga kuwajengea uwezo wananchi jambo ambalo ni chachu ya maendeleo yaliyokusudiwa na serikali.

Waziri wa Wizara hiyo, Riziki Pembe Juma, alisema hayo jana akiwa kwenye ziara katika Chuo cha Wajasirimali Wanawake cha Bare Foot Collage kilichoko Kinyasini Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema lengo la ziara yake ni kujifunza na kuona jitihada zinazofanywa na wanawake katika jamii, hivyo wizara itaendelea kushirikiana na ZEEA katika kuwapatia wanawake fursa na kuondokana na ugumu wa maisha.

Waziri Riziki alisema kila mwanamke ni kiongozi katika familia, hivyo serikali itaendelea kuwaunga mkono wanawake na kuwashauri wajasirimali wanawake kutovujinka moyo na kuzikabili changamoto wanazokutana nazo katika shughuli zao na kusisitiza kwamba hakuna mafanikio yasiyo na changamoto.

Aidha, Riziki aliwataka wanaume kuwaruhusu wake zako kwenda kujifunza ujasiriamali na kubainisha kwamba kumekuwa na malalamiko kwa baadhi ya wanawake kutokupewa ruhusa na waume zao. Alisema hali hiyo inawarudisha nyuma wanawake kuleta maendeleo katika jamii.

Naye Mkurugenzi wa Bare Foot Collage, Brenda Ndossi, alisema taasisi hiyo itaendelea kutoa elimu kwa wanawake ambao hawana ujuzi wowote ili kuwa na uwezo wa kusaidia jamii.

Mwezeshaji katika kituo hicho, Miza Juma Othman, aliishukuru serikali kwa kuwaka mazingira mazuri ya kuwakomboa wanawake kimaisha, na kuiomba serikali kuendelea kuwaunga mkono wanawake hao waweze kufanya kazi kwa ufanisi.

Mmoja wa wanafunzi waliopatiwa ujuzi, Fatma Haji Machano, kutoka Shehia ya Zingwezingwe, aliwataka wanawake wengine ambao hawana kazi wala ujuzi kujiunga na kituo hicho ili kuondokana na umaskini.

Bare Foot College ina wanafunzi 21 wakiwamo 12 kutoka Zanzibar na tisa kutoka Somalia wanaojifunza utengenezaji wa taa za kutumia umeme wa jua.

Chuo hicho pia kinatoa ujuzi wa fani tofauti zikiwamo ufugaji nyuki, ushoni na elimu ya kilimo na tayari kimeshatoa wanafunzi 1,054 katika fani tofauti.

# Mwinyi aonesha utayari ushirikiano na shirika la uendeshaji bandari Indonesia

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali iko tayari kushirikiana na Shirika la Pelindo kujenga Bandari Jumuishi ya Mangapwani ambayo itajumuisha sehemu ya kuhifadhi nafaka, makontena, bandari kavu, chelezo na hifadhi ya mafuta.

Pia bandari hiyo inatarajiwa kuwa kituo cha kuhudumia eneo la ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana alipotembelea Bandari ya Tanjung Priok, Jakarta nchini Indonesia na kukutana na uongozi wa Pelindo, shirika linalomilikiwa na serikali ya nchi hiyo ambalo linaendesha shughuli zote za bandari nchini humo.

Rais Dk. Mwinyi alisema anatambua kuwa Indonesia na Zanzibar zinafanana kwa kuwa ni nchi za visiwa na hutegemea bahari kwa shughuli za uchukuzi.

**Rais Dk. Mwinyi alisema anatambua kuwa Indonesia na Zanzibar zinafanana kwa kuwa ni nchi za visiwa na hutegemea bahari kwa shughuli za uchukuzi.**

Pia alisema muundo huo wa kijiografia wa visiwa una changamoto mbalimbali za usafirishaji, hivyo bandari inachukua nafasi muhimu katika kutatua changamoto za kibiashara na kuchochea kukua kwa uchumi wa nchi.

Arif Suhartono, Mkurugenzi Mkuu wa Pelindo yenye matawi 71 nchini humo, ikijumuisha kisiwa cha Sumatra kwa upande wa magharibi hadi mashariki ya Papua New Guinea, alisema ziara hiyo iwe mwanzo wa ushirikiano wa karibu zaidi na kuweka msingi wa ushirikiano wa kimkakati kati ya Indonesia na Zanzibar.

Rais Dk. Mwinyi amekamilisha ziara yake nchini humo iliyoanzia Septemba Mosi hadi 3, mwaka huu, katika kisiwa cha Bali.




Katibu Mkuu wa Chama Cha Wafugaji Tanzania (CCWT), Mathayo Daniel (kushoto) na Mkuu wa Kitengo cha Mikakati wa Benki ya NBC, Msafiri Shayo wakionesha hati jijini Dar es Salaam juzi, baada ya kutiliana saini makubaalino baina ya taasisi hizo yanayolenga kufungua milango kwa benki hiyo, kutoa huduma za kifedha zenye upendeleo maalum kwa wafugaji na wadau waliopo kwenye mnyororo wa sekta hiyo nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SMZ, wadau bega kwa bega kuboresha afya

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) itaendelea kutoa ushirikiano na mashirika mbalimbali ya kimataifa katika kuwaletea maendeleo wananchi.

Ushirikiano huo ni pamoja na kuimarisha afya ya mama na mtoto kwa maslahi mapana ya wananchi wa Unguja na Pemba.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na uongozi wa Shirika la Kimataifa la D- TREE ( Dtree International ) ambalo linafanya kazi kwa kushirikiana na Wizara ya Afya Zanzibar hasa kwenye huduma za afya ya jamii, uliofika ofisini kwake, Vuga, kwa lengo la kujitambulisha.

Hemed alisema kuwa serikali itaendelea kutoa kila aina ya ushirikiano kwa shirika hilo ili kufanya kazi zake kwa ufanisi katika kuwapatia elimu wafanyakazi wa afya hasa wale wa vijijini ili kutoa huduma bora kwa kila mwananchi.


Kwa mujibu wa Hemed, mpango ambao shirika hilo limekuja nao wa kuwapatia elimu wafanyakazi wa kujitolea (CHV) katika afya, utasaidia kwa kiasi kikubwa kupiga hatua za kimaendelea kwa sekta hiyo kwa maslahi ya wananchi wa Unguja na Pemba.

Hemed alisema serikali itaendelea kuwapa kipaumbele wafanyakazi wanaojitolea katika sekta ya afya ili kuhakikisha wanatoa huduma bora kwa wananchi hasa wale wa vijijini ikiwamo kutoa elimu ya kujikinga na maradhi yasio ya kuambukiza kama vile kisukari na shinikizo la damu.

Mkurugenzi Mtendaji D -Tree Zanzibar, Riccardo Lampariola, aliishukuru SMZ kwa kuendelea kuwaamini na kufanya nao kazi hasa katika huduma za afya ya jamii.

Alisema kwa sasa shirika limeandaa programu ya kufanya kazi kwa njia ya kijiditali ambayo itawasaidia wafanyakazi wa afya hasa wale waanojitolea kufanya kazi kwa urahisi na kutoa huduma bora kwa wananchi wote.

Pia alisema kwa kushirikiana na jamii ya Wazanzibari, anaamini malengo ya shirika ya kutoa huduma bora kwa wafanyakazi wa afya kwa wilaya zote za Unguja na Pemba yatafikiwa kwa ufanisi zaidi.



**CHIDIMA**

UKURASA 14

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# BT
## BURUDANI TELE





# JUX KAPAKI BASI

NYOTA wa muziki wa kimahaba, Juma Jux, amezidi kugonga vichwa vya watu baada ya kumtangaza mpenzi wake mpya mrembo kutoka Nigeria, Priscilla Ololufemi.

Priscilla ambaye kimwonekano ni mrembo na mwenye tabasamu kila mara, amewaweka njia panda mashabiki wa mwanamuziki huyo kujua kama ameweza kuziba nafasi ya Vanessa Mdee.

Jux tangu alipoachana na Vanessa, amekuwa akibadilisha wanawake kila mara  kitu ambacho kinadaiwa na wengi kwamba bado alikuwa akisumbuliwa na 'mzimu' wa mrembo huyo ambaye tayari ameolewa na mwigizaji  kutoka Nigeria.

Katika mahojiano yake ya hivi karibuni, Jux amesema kwamba kwa sasa ana furaha baada ya kukutana na Priscilla na alitamani kama angejitokeza mapema.

"Natamani tungekutana mapema," amesema kupitia mtandao wa kijamii.

Miezi mitano iliyopita, Jux alikuwa katika uhusiano na Karen Bujulu ambaye walibwagana katika hali isiyotarajiwa.

Hata hivyo, mashabiki wake wengi wanajiuliza kuwa Priscilla ataweza kuziba nafasi ya Vanessa na kusababisha mwanamuziki huyo kutulia kama anavyosema mwenyewe?

Jibu analo mwenyewe Jux, ambaye tayari amewahakikishia kuwa kwa Priscilla ameshafika safari yake kwa sababu anajiona mwenye bahati kuwa naye.

BASI SAWA

## Mc Pilipili hawahofii Gen Z



MSANII wa uchekeshaji, Mc Pilipili, amesema hawezi kuwahofia vijana wanaochipukia katika sanaa hiyo kwa sababu yeye ni mkongwe na amejiwekea mizizi.

Amesema kwamba Sanaa ya uchekeshaji majukwaani huko nyuma haikuwa na umaarufu, lakini kutokana na juhudi zake aliweza kupeleka maonesho mikoani na kupokelewa na watu wengi.

"Mimi ndio mchekeshaji pekee ambaye nilianza kupeleka shoo mikoani tangu nchi ipate Uhuru, kwa hiyo vijana kwangu sawa na wajukuu zangu hawawezi kunipa hofu wala hawanishtui kabisa," amesema Mc Pilipili.

## Rupia Boytz kuachia 'Zigo' kesho



MWANAMUZIKI chipukizi wa kizazi kipya, Salim Mkilindi, maarufu kama Rupia Boytz, amejiandaa kuachia singo yake ya kwanza inayoitwa 'Zigo' kesho usiku.

Akizungumza na BT jana, Rupia Boytz, amesema kwamba kazi hiyo ni ya kwanza kuitambulisha kwa mashabiki wa muziki na kwamba imetayarishwa katika ubora unaokubalika.

Amesema wimbo huo ambao umerekodiwa katika studio ya High table ya Barnaba na video yake imeongozwa na Jimmy, utakuwa ni mmoja wa nyimbo bora kutoka kwa wasanii wanaochipukia mwaka huu.



## MARIOO AWATUPIA JIWE WANAOMCHIMBA

MWANAMUZIKI nyota wa Bongo Fleva, Marioo, amewatupia mawe watu wanaomfuatilia katika penzi lake na Paula, akisema wataishia shimoni.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Marioo aliandika sehemu ya shairi la wimbo wa msanii wake Stans, huku akisema watu hao sawa na pweza wanaotabiri mapenzi ya watu.

"Ujumbe huu uwaendee wote wenye tabia ya kutabiri mapenzi ya watu, hao wanaojifanya pweza wa kutabiri penzi mwaka huu tuwachinje tunywe chuzi la kuongeza nguvu, watashindwa," ameandika Marioo.





## Mwijaku eti hamuogopi Vunjabei

MWIGIZAJI na mtangazaji, Mwijaku, amemjibu Fredy Vunjabei akisema hana wasiwasi na kile alichokisema na kwamba haogopi kufunguliwa kesi.

Hivi karibuni kumekuwepo na majibizano Mwijaku aliibua majibizano makali baada ya kumwambia Diamond Platnumz hawezi kuwa tajiri namba moja kwa sababu utajiri wake hauwezi kumfikia Vunjabei.

Hata hivyo, Vunjabei alijitokeza na kumpiga marufuku Mwijaku kujihusisha na kazi zake.

"Vunjabei namjua ni mwoga, alipomsikia Diamond anataka mdahalo wa wazi kuonesha utajiri wao ndio maana ananitishia, lakini mimi siogopi vitisho," amesema Mwijaku.

## WASANII WALIVURUGWA AGOSTI

**Na Adam Fungamwango**

UNAWEZA kusema kuwa mwezi Agosti wasanii wa bongo fleva walivurugwa. Walipishana studio kurekodi na kufyatua ngoma. Ulikuwa ni mwezi ambao wasanii wengi walitoa ngoma zao, kuanzia wale mastaa, wakongwe na waliofanya vizuri kwenye gemu.

Ngoma zaidi ya 10 zilirekodikwa kwa mwezi huo tu kitu ambacho si cha kawaida sana.

Leo hii tunawaletea kwanza ngoma tano, halafu woki ijayo tutawaletea zingine tano ambazo zilitolewa mwezi Agosti na kwa sasa zimeanza kutamba na kuwa gumzo kwenye redio, televisheni na mitandao ya kijamii.

Ngoma tano leo zitawahusu wasanii wale ambao ni mastaa zaidi.

**Harmonize - Sherehe**

Tunaanza na Tembo, Harmonize ambaye mwishoni mwa mwezi Agosti, ikiwa ni siku tano tu kabla ya kumalizika kwa mwezi huo alifyatua ngoma yake akaiita, 'Sherehe.'

Yeye anasema wakati kuna watu wengine mapenzi yanawatesa kwao wao ni sherehe. Ngoma hii imetoka Agosti 25 kwa mtindo wa video.

**Alikiba ft Billnass - Fallen Angel**

Agosti 10, msanii nyota Ali Kiba akatoa ngoma yake, 'Fallen Angel, aliyomshirikisha Billnas. Si mara kwa mara Kiba kutoa ngoma, lakini mwezi Agosti hakuwa nyuma.

**Marioo - Iphone Users**

Mapema kabisa, Agosti 7, msanii Marioo alifyatua ngoma yake, akaiita 'Iphones User.' Ni ngoma ambayo mapigo yake ni ya kuchezesha zaidi na haipo kwenye madhadhi ya zile ngoma za mahaba.

**Whozu - Mii**

Whozu naye hakuna nyuma, alitoa ngoma ya 'Mii', Agosti 9. Ni ngoma ya mapenzi ya kubembeleza, ambayo kwenye picha yake ya video, msanii huyo amepiga picha na timu ya warembo waliojipamba kwa mavazi ya harusi wakiwa wameshika maua ya waridi rangi nyekundu na nyeupe.

**Madee - Mwizi**

Ni wimbo wa masikitiko, uliotolewa Agosti 14 na msanii Madee, ukionyesha jinsi wananchi wanavyohangaika kutafuta pesa, lakini mwisho wa siku wanaishia kuitwa wezi wakati siyo kweli.

Baadhi ya mashabiki wa bongo fleva, wananasibisha wimbo huo na tukio lililompata msanii Mandojo hivi karibuni ambaye licha ya kuwa raia mwema, tena ni staa, lakini akaitiwa kelele za mwizi, akapigwa hadi kuuawa.




FILAMU

# Malkia mweupe mwokozi



**Na Adam Fungamwango**

FILAMU hii kali na yenye mafunzo, itaitwa, 'Malkia Mweupe.' Maudhui yake yanalenga kuonesha baadhi ya watu kwenye jamii waliojifanya wao ni wababe, wakionea watu kutokana na uwezo wa pesa, madaraka, vyeo na vitu vingine vinavyofanana na hivyo.

Wengine wanajigamba kwa nguvu za kishirikina walizonazo na kuwatia hofu watu wanaomzunguka ili kuogopeka na kupata heshima asiyokuwa nayo.

Waliocheza filamu hii ni Adili Iddi, Maria Wambura, Aisha Mussa, Deo Michael, Zema Mkima, Hamisi Akamwela, Smaiya na Frank.

Picha linaanza kwa kijana mmoja kaka yake Zubeda, aliekwenda kumsalimia dada yake, lakini kwenye kijiji hicho anakutana na sheria moja kali, kuwa ni lazima amheshimu mtu mmoja anaitwa mzee Mkima.

Hakufanya hivyo akawa mkaidi, kilichompata ni kuteswa kiuchawi na mzee Mkima kwa usiku mzima.

Ili aendelee kuwa hai, adhabu nyingine aliyopewa ni dada yake kukaa kwa siku saba kwa mzee Mkima kama hawara yake.

Mzee Mkima, nguvu zake cha kishirikina anawafanya wanakijiji kuwa waoga, kiasi kwamba anawalazimisha akipita wasiongee chochote wanyamaze tu. Na akipita wakinyamaza pia ni kosa.

Akikuta mtu njiani amenunua nyama anapeleka kwao analazimishwa apeleke kwake. Ili mradi tu wanakijiji wanapata mateso ya kuteswa kwa uchawi, na uonevu bila msaada wowote.

Kijijini anaingia kijana mmoja aitwaye Faridi, aliyetoka mjini kuja kusalimia ndugu zake.

Wanamsimulia awe makini na mzee huyo aitwaye Mkima. Asubuhi anakwenda mtoni kunawa, anakutana na chupa iliyofungwa na kitambaa chekundu anaifungua.

Siku mbili baadaye anakutana na mzee Mkima ambaye anamuonesha kuwa yeye ni nani kwa sababu amemchukulia mpenzi wake. Faridi anashangaa. Asubuhi anaamka anamkuta mchawi ambaye ni mzee Mkima ameganda mlangoni mwake. Anawapigia simu rafiki zake ambao wanaita kundi la wanakijiji na kuanza kumpiga, wengine wakitaka kumuua, mwishowe wakaamua kumpeleka polisi.

Kesho yake Faridi anakwenda tena mtoni, anatokewa ghafla na msichana mrembo mweupe. Anamwambia asituke hawezi kumdhuru. Akamwambia kuwa yote yaliyotokea kwa mzee Mkima kushindwa kumroga na hatimaye kunasa ni yeye ndiye alifanya hivyo. Na alikuwa analipa fadhila kutokana na kumfungua kutoka ndani ya chupa aliyofungwa muda mrefu. Akamwambia awali alikutana na mzee Mkima baada ya kutoka kwenye chupa na akamtamani kumuoa, lakini akamwambia yeye ni mchumba wa Faridi, ndipo mzee huyo alipokasirika na kutaka kumuua.




# Chidimma akumbuka maumivu Afrika Kusini

MSHINDI wa Miss Universe wa Nigeria, Chidimma Adetshina amesema amepitia machungu kutokana na kutokubalika wakati wa shindano la Miss Afrika Kusini.

Adetshina ambaye hivi majuzi alitawazwa kubeba taji hilo nchini Nigeria, amesema jina lake lilimfanya abaguliwe na Waafrika Kusini kwa kumwona sio mwenzao.

"Yote yalianza kwa sababu ya jina langu, watu hawakufurahi jina langu Chidimma ninawakilisha Afrika Kusini, na hapo ndipo ilipoanzia. Waafrika Kusini walihisi kama mimi si mwenzao kwa sababu tu ya jina langu. Ilikuwa tukio la huzuni," amesema Adetshina.



## Seun amsifia baba yake Fela Kuti

MWANAMUZIKI wa Nigeria Seun Kuti, amefunguka kuhusu uhusiano wake na baba yake Fela Kuti, akielezea kama kushinda bahati nasibu.

Akiongea hivi karibuni, msanii huyo mwenye utata amesema maisha yake na baba yake ni sawa na furaha ya ushindi wa mchezo huo wa kubahatisha na kwamba anajivunia daima.

"Nani huwa anakasirika akishinda bahati nasibu? Nioneshe mtu mmoja ambaye alishinda siku moja na kusema ana hasira, sawa na mimi nimekuwa mshindi," alisema huku akicheka.

## Spyro kumbe alikuwa kiwembe

MSANII nyota wa muziki kutoka Nigeria, Spyro amekiri kwamba amekuwa katika mapambano ya kuacha ngono kutokana na kumsababishia matatizo mengi katika ndoa yake.

Alikiri kuwa kabla hajajikita katika imani na kumjua Mungu alishiriki mapenzi na wanawake tofauti na kumletea athari.

Mwimbaji huyo, alisema kila mara aliposhiriki ngono nje ya ndoa, alihisi hali ya kutoridhika na kusababisha kutamani kuendelea na wanawake wengine.





## Krane sasa umejifunza

BAADA ya kuachiwa kutoka rumande kutokana na madai ya kumkashifu Davido, mwimbaji wa Nigeria Dammy Krane, ameomba radhi kwa mashabiki wake.

Krane aliandika kupitia ukurasa wa X, kuwa anajutia matendo yake na kuelezea mipango yake ya kusonga mbele kimuziki.

"Samahani kwa kila kitu, kwa mashabiki wangu, ninamatumaini bado ninao, samahani sana na sasa nasonga mbele, tarajia muziki mzuri kutoka kwangu na muziki pekee nawapenda," ameandika.

## Omori matumaini bado yapo

MASHABIKI wa mwongozaji maarufu wa video za muziki nchini Nigeria, TG Omori wamefurahi kupata taarifa kuhusu kuendelea vizuri kwa afya yake baada ya zoezi la kupandikiza figo kushindikana.

TG Omori aliandika kwenye ukurasa wa X kwamba mchakato wa kupandikiza figo nyingine unakwenda vizuri na aliwashukuru wote wanaomwombea dua.

"Asanteni nyote kwa maombi na kunitakia heri, ninapona sasa kutoka kwenye mshono wa kwanza ulioshindikana, nitaendeleza mapambano," ameandika







Mkuu wa Shule ya Sekondari Endasak, wilayani Hanang' mkoani Manyara, Rogate Munisi (wanne kushoto) na Makamu Mkuu wa Shule ya Sekondari Mirerani B.W. Mkapa, Thomas Senteu wakiweka shada la maua kwenye kaburi la Lidya Saitoti mmoja kati ya wanafunzi watatu wa Endasak waliofariki kwenye ajali iliyotokea Gawal, wilayani Babati Agosti 31 mwaka huu, wakati wa maziko yaliyofanyika Mirerani juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Vijiji vyawekewa mkakati ushiriki demokrasia

**Na Godfrey Mushi,** HAI

VIJIJI vya Kwa Sadala, Mungushi na Kware vilivyoko Kata ya Masama Kusini, Hai mkoani Kilimanjaro, ambavyo mwaka 2020 vilionesha ushiriki hafifu wa raia katika Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani, vimeundiwa mkakati maalum kuchochea ushiriki wa masuala ya utawala, uchaguzi, kupambana na ufisadi na rushwa.

Mradi wa 'Maendeleo Yetu' unaotekelezwa kwa ubia, kati ya Shirika la Tusonge CDO na Taasisi ya Uwajibikaji wa Umma (WAJIBU), unatazamia kufanya kazi hiyo katika Mkoa wa Kilimanjaro katika kipindi cha mwezi Septemba hadi Novemba mwaka huu, kwa awamu ya kwanza.

Akizungumza jana wakati wa kikao cha kwanza na wadau wa serikali katika kata hiyo, Meneja Programu wa Tusonge CDO, Lawi Msemwa, alisema mradi huo unatekelezwa katika mikoa 15 Tanzania na mashirika tofauti 157.

"Malengo ya mradi huu ni kuwawezesha wanawake, watu wenye ulemavu na vijana, ambao ni raia wa Tanzania katika maeneo ya mradi kuweza kushiriki katika utawala, uchaguzi na kupambana na ufisadi na rushwa.

"Pia kuboresha uwazi, uwajibikaji na ushiriki wa raia katika uchaguzi unaokuja na kuchochea mazingira ya uongozi na utawala unaowajibika," alisema.

Matokeo tarajiwa ya mradi huo ni wananchi wenye nguvu (wanawake, vijana na wenye ulemavu) wanashiriki kikamilifu katika michakato ya uchaguzi, ikiwemo mijadala ya sera, usajili wa wapiga kura na kupambana na ufisadi.

**"Pia kuboresha uwazi, uwajibikaji na ushiriki wa raia katika uchaguzi unaokuja na kuchochea mazingira ya uongozi na utawala unaowajibika," alisema.**

Yamo pia masuala ya uwazi na uwajibikaji ulioboreshwa kupitia kuimarisha sheria na kanuni, pamoja na ushirikishwaji wa vyombo vya habari katika mchakato wa uchaguzi.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Masama Kusini, Rose Mengo, aliishukuru Tusonge CDO, kwa kuwapelekea mradi huo ili kuamsha ari ya wananchi wa vijiji vya Kwa Sadala, Mungushi na Kware, kupata elimu ya mpiga kura na kuhamasika kujiandikisha katika daftari la kudumu la mpiga kura.

Alisema Kata ya Masama Kusini ina kaya 4,899 zenye watu 18,524 wakiwamo wanaume 9,063 na wanawake 9,461 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022.

Aidha, Mtendaji Mengo alisema kijiji cha Mungushi kina kaya 1,367 zenye watu 5,084, wanaume wakiwa 2,632 na Kware ina na kaya 438 zenye watu 1,753 wakiwamo wanaume 928 na wanawake 825, wakati kijiji cha Kwa Sadala chenyewe kinazo kaya 2,492 zenye watu 9,379 wanaume 4,555 na wanawake 4,824.

Gilbert Owen, Ofisa Ufuatiliaji na Tathimini wa Shirika hilo, alisema walengwa wa mradi huo wa utoaji wa elimu ya mpiga kura, ni wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wenye umri wa miaka 18 hadi 35 na kuendelea, kwa kuwa sensa ya mwaka 2022 inaonesha kuwa asilimia 51.3 (sawa na watu 30,713,709) ni wanawake.

Huku asilimia 34.4 sawa na watu 20,612,566 ni vijana, na watu wenye ulemavu nchini ni zaidi ya milioni 3.3

# Wadaiwa kuhujumu mradi wa maji

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WANANCHI wa Kijiji cha Sango, Kata ya Kimochi, Moshi mkoani Kilimanjaro, wamedaiwa kuhujumu mradi wa maji uliofanyiwa maboresho makubwa ya miundombonu na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Moshi (MUWSA), kwa madai ya kupinga kufungiwa dira za maji na kulipa ankara.

Uchunguzi wa awali, umeonesha miundombinu iliyoharibiwa vibaya ina gharama ya zaidi ya Sh.milioni 14.

Kutokana na uhujumu huo, Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kamishina Jenerali Mstaafu James Kaji, amegiza Mkuu wa Polisi wa Wilaya hiyo , kuwasaka na kuwatia mbaroni wananchi wote waliofanya uharibifu wa miundombinu hiyo.

Kaji alisema bila kujali gharama zilizotumiwa na serikali, wananchi hao kwa makusudi wameng'oa mabomba ya vyuma ya mradi huo, kuvunjavunja visima, chemba tisa za kupunguzia kasi ya maji, kutoboa visima vidogo na kung'oa mabomba yaliyolazwa kwenye mitaro.

Pia, alisema wako waliovunja miundombinu hiyo mchana na wengine usiku, hivyo wote watafutwe na hatua za kisheria zitachukuliwa ili kukomesha vitendo vya aina hiyo.

"Watu hao wakamatwe mara moja, hawa ni sawa na wauwaji, wamekata mabomba, kuvunja miundombinu ya maji iliyopita kijijini kwao kisa hawataki kufungiwa mita, na maji yamepungua, hili halivumiliki, na niwaombe wananchi kuhakikisha wanafuata sheria taratibu na kanuni za nchi," alisema Kaji

Wakati huo huo, Kaji aliitaka MUWASA kuhakikisha wanawashirikisha wananchi kabla ya kufanya jambo lolote ili kujenga uelewa wa pamoja na kuwatumia katika kazi zinazohitaji vibarua.

"Umekuja kuweka bomba washirikishe kwa nini unaweka hilo bomba na faida yake, unakuja kusafisha kisima toa taarifa. Na nyinyi wananchi mkiitwa kwenye vikao hakikisheni mnafika ili kupata maelekezo na maagizo ya serikali,"alisisitiza.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MUWASA, Tumaini Marandu, alisema lengo la mradi huo, ni kuhakikisha licha ya mabadiliko ya tabianchi ila kila mwananchi aweze kupata maji hata kwa mgao.

"Licha ya jitihada hizo, tumekuwa tukipata upinzani mkubwa kutoka kwa wananchi na hata wakati mwengine mafundi hutishiwa maisha. Hawataki kufungiwa dira na kulipia maji, na badala yake wanataka kutumia maji bila malipo.

"Septemba 2, mwaka huu, waliamua kuharibu miundombinu hiyo kwa kutindua mabomba na kuvunja chemba za kupunguzia kasi ya maji wakishinikiza kutofungiwa mita," alisema Marandu

Alisema uchunguzi wa awali ulionyesha miundombinu ya zaidi ya Sh.milioni 14 imeharibiwa.

"Tumepokea malekezo kutoka kwa mkuu wa wilaya, tunaenda kukaa na viongozi wa vijiji hivyo katika kuhakikisha maji yanarejeshwa katika kijiji hicho,"alisema.

# Mnyika asisitiza wananchi kushiriki uchaguzi wa mitaa

**Na Steven William,** MUHEZA

KATIBU Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika, amewataka viongozi na wanachama wa chama hicho kujipanga ipasavyo kushiriki kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa ili kuongoza vijiji, vitongoji na mitaa nchini.

Akizungumza jana katika mkutano wa hadhara uliofanyika uwanja wa Majengo Shimoni, Muheza mkoani Tanga, Mnyika alisema viongozi na wanachama wanapaswa kujiandaa ili washiriki na kushinda nafasi za uchaguzi huo Novemba 27 mwaka huu.

Alisema ushindi wa nafasi hizo kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa, utakuwa mwanga na dira ya ushindi wa uchaguzi mkuu wa nafasi ya Urais na Wabunge na Madiwani, unaotarajiwa kufanyika mwaka 2025.

Mnyika alisema wananchi wa Muheza, wanatakiwa ifike mahali sasa kuacha uteja wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na badala yake waikatae.

Pamoja na mambo mengine, alisema kuwa serikali ya CCM imeleta ugumu wa maisha, kwa kupanda kwa gharama za maisha kwa wananchi hasa kwa bidhaa muhimu, ikiwemo sukari.

Alisema serikali ya Rais Samia Suluhu imeweza kukopa fedha nyingi kuliko marais wenzake wote waliopata nchi hii na kwamba mzigo wa kulipa hilo deni watabebeshwa wananchi.

Aliwaonya watendaji wa serikali kuacha mara moja tabia ya kuibeba CCM katika uchaguzi na kwamba CHADEMA wapo macho kuhusu hilo.

Mnyika aliwaomba wananchi wa wilaya ya Muheza kwa jumla kuendesha maombi kwa Mungu ili kuibwaga CCM ambayo imekuwa ikileta vikwazo kuwapa shida za maisha wananchi katika nchi yao yenye utajiri mwingine wa mali lakini wananchi masikini wanafaidika viongozi.

Awali, Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Kanda ya Kaskazini, Yosepha Komba, alisema kuna baadhi ya viongozi wa CCM wanawatuma vijana wao kuteremsha bendera za chama hicho usiku.

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# ZAMA ZIMEBADILIKA!

## -Kijora pambe, dera vimegeuka kadi siku hizi ya kuingia kwenye ukumbi!

Na Adam Fungamwango

KILA kukicha mambo yanabadilika. Kila zama na kitabu chake. Kitu ambacho wengi hawakijui ni kwamba kule uswahilini hivi sasa mambo ya kwenda ukumbini na kadi yameanza kwisha.

Hivi sasa akinamama hawaalikani kwa kadi kama ilivyokuwa miaka kadhaa nyuma. Hivi sasa mambo ni mwendo wa vijora pambe na madela tu. Wanaalikana vipi, endelea kusoma.

Imezoeleka kuwa watu wanaalikana kwa kadi ya mchango na mwaliko. Mtu anakuletea kadi kama ana sherehe yake yoyote ile iwe siku ya kuzaliwa, ubatizo, maulidi, unyago, kipaimara, komunio, au kutunzana kwa kinamama.

Halafu ile kadi inaandikwa kiasi cha mchango unaotakiwa, au wowote ule uliojaaliwa kuwa nao. Mara nyingi kadi ya mchango hufuatana na ya mwaliko kwa aliyetoa, ambapo yeyote aliyenayo anatakiwa kuionesha tu mlangoni ndipo anaporuhusiwa kuingia ukumbini.

Bila kadi hiyo huwezi kuingia kwani mlangoni unakutana na mabaunsa na sura zingine ambazo ni tofauti na ulizozoea. Uliowazoea utawakuta ndani kama ukiingia.

Mtindo huu ndiyo uliozoeleka mpaka sasa. Na huu ulianza mwishoni mwa miaka ya 1990 na mwanzoni mwa miaka ya 2000, ambapo awali ilikuwa tofauti.

Zamani sherehe zote zilikuwa zinafanyika nyumbani. Mtu akiwa na sherehe yake yoyote ile kama nilivyozianisha hapo juu.

Mtu anapoalikwa moja kwa moja anakwenda nyumbani kwa aliyemualika ambako ndipo sherehe hufanyika na ilikuwa hivyo miaka yote kwa miaka hiyo kuelekea nyuma.

Hakuna aliyefanya sherehe ukumbini, badala yake kula, kunywa na muziki vyote vilifanyika kwa mhusika mwenyewe.


Kwa sasa si hivyo tena, kwani watu wameacha kufanyia sherehe hizo nyumbani, badala yake hukodi ukumbi.

Unaweza kualikwa na mtu na ukaenda kwenye sherehe yake hata nyumbani kwake hukujui. Labda uwe rafiki yake mliyeshibana. Badala yake utakwenda kwenye sherehe yake na kufurahia bila kujua hata anapoishi, ili mradi tu mnafahamiana, mfanyakazi mwenzako, au jamaa tu.

Hali hii nayo sasa naona kama inaanza kufifia taratibu na kama itaendelea huko mbele tunaweza kusema mengineyo.

Imeanza kwa akinamama.





Siku hizo madera na vijora pambe ndiyo vimekuwa kama kadi ya kuikingilia ukumbini.

Mlangoni mabaunsa wanakuwa wameshaambiwa na kupewa aina ya sare zinazotakiwa huko ukumbini. Bila hivyo utaishia nje. Sare inaweza kuwa moja, mbili au hata tatu, inategemea na mwenyewe jinsi alivyoandaa.

Mwenye sherehe anakuwa anatembeza sare hizo za vijora na madera kwa mashoga zake, ndugu na jamaa. Anakuwa na mzigo wa vijora na madera akitembeza na kugawa, ama kwa pesa kamili au ahadi. Anayeshindwa mzigo unakuja kuchukuliwa kabla ya sherehe na ukitimiza, basi siku hiyo mtu anavaa kwenda ukumbini. Ukionekana tu mlangoni unaruhusiwa.

Mvaaji akishapewa na mhusika, anatakiwa kutoa kuanzia Sh 8,000, hadi 15,000 kutegemea na sherehe na ubora wa vijora.

Aliyeandaa sherehe hunufaika kwa kutembeza vijora hivyo kwa sababu anakuwa amekwenda dukani na kununua kwa pesa ndogo kidogo na yeye akija kwa wenzake anazidisha bei.

Mfano akinunua vijora 30 kwa Sh. 5,000, atavigawa na Sh 8,000, na kama akivipata kwa Sh 6,000 au 7,000, atavitembeza kwa wenzake kwa Sh 10,000, na faida itakayopatikana ndiyo ya kwake.

Pesa ya ziada anayoipata inamsaidia kupunguza kama si kumaliza kabisa gharama za uendeshaji wa sherehe.

Hivyo ndivyo kinamama wa uswahilini kwa sasa amavyofanya. Hii inaweza kusababisha hata kinababa nao wakafanya hivyo kwa kutembezeana sare za fulana au mashati.

Wanawake wa uswahilini wako sahihi kwenye hili walilovumbua? Msomaji tunaomba maoni yako na tutayachapisha kwenye toleo linalofuata wiki ijayo.

**Tuma meseji 0716 350534.**

## Afungwa miaka 20 kusaidia mauaji ya kimbari Rwanda

**KIGALI, Rwanda**

MAHAKAMA nchini Rwanda imemuhukumu, Venant Rutunga, kifungo cha miaka 20 jela baada ya kupatikana na hatia ya mauaji ya kimbari ya mwaka 1994.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari nchini humo, vilisema Rutunga mwenye miaka 75, alirudishwa Rwanda kutokea Uholanzi 2021, alikutwa na hatia ya kuagiza kufanyika mauaji hayo.

Kulingana na mwendesha mashitaka, Rutunga aliwapeleka polisi kwenye taasisi ya utafiti wa kilimo kulikokuwa na wafanyakazi wa Kitutsi na watu wengine waliokuwa wamejificha, ambao wote waliuawa.

Rutunga aliwahi kuwa mkurugenzi wa kikanda wa taasisi hiyo ya ISAR.

Hata hivyo, alikana mashtaka hayo akieleza kuwa aliwaita maofisa hao ili kulinda usalama, uamuzi ambao alisema uliidhinishwa na bodi ya wakurugenzi ya ISAR.

**DW**

## Watu watano wauawa ukingo wa Magharibi

**TEL AVIV,** PALESTINA

WAPALESTINA watano wameuawa katika shambulizi la anga lililofanywa na Israel kaskazini mwa Ukingo wa Magharibi unaokaliwa kwa mabavu.

Wizara ya afya ya Palestina ilisema watu wengine wawili walijeruhiwa katika tukio la gari kushambuliwa katika eneo la Tubas juzi.

Jeshi la Israel lilisema lilishambulia kikundi cha kigaidi kilichokuwa na silaha na kudai waliouwa walikuwa wapiganaji.

Vyombo vya habari vya Palestina pia vilisema mvulana mwenye umri wa miaka 16 aliuawa kwa kupigwa risasi na wanajeshi wa Israel katika kambi ya wakimbizi ya al-Faraa.

Hata hivyo, taarifa ya jeshi hilo ilisema vikosi vilimuua gaidi ambaye alikuwa na kilipuzi katika majibizano ya risasi na kwamba shambulio hilo lililenga wengine.

Kwa muda wa siku tisa, wanajeshi wa Israel wamekuwa wakivamia miji ya kaskazini ikiwa ni sehemu ya kile wanachosema ni operesheni kubwa ya kukabiliana na ugaidi.

Wizara ya Afya ilisema jumla ya Wapalestina 36 wameuawa, wakiwemo 21 kutoka mkoa wa Jenin na wanane Tubas.

Madai kuwa wengi wa waliofariki ni wanamgambo makundi yenye silaha , yanakanushwa na wizara hiyo ambayo ilisema watoto kadhaa pia ni miongoni mwao.

Aidha, mwanajeshi mmoja wa Israel aliuawa wakati wa mapigano yaliyotokea Jenin.

Taarifa kutoka kwa Jeshi la Ulinzi la Israel (IDF) ilisema wanajeshi na jeshi la Magereza la Israel walianza operesheni katika kambi ya Tubas na al-Faraa Jumatano usiku.

Ilimtaja mmoja wa watu watano waliouawa katika shambulio la anga huko Tubas kuwa ni Mohammed Zakaria Zubeidi, ambaye ilidai alikuwa gaidi kutoka eneo la Jenin.

Pia aliyeuawa ni mtoto wa Zakaria Zubeidi, kamanda wa zamani wanamgambo wa harakati ya Fatah, Brigedi za Mashahidi wa Al-Aqsa.

**BBC**

## Zelensky aomba silaha zaidi kuishinda Russia

**KYIV,** RUSSIA

RAIS wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, amehudhuria mkutano wa kundi la kimataifa linaloungа mkono nchi yake na kuyataka kutoa msaada zaidi wa silaha katika kupambana na Russia.

Mkutano huo unafanyika katika kambi ya kijeshi ya Marekani ya Ramstein iliyoko Ujerumani.

Kwenye mkutano huo, Rais Zelensky aliwataka washirika wake hao kuongeza silaha ili kuwaondosha wanajeshi wa Russia ndani ya ardhi yao.

Kiongozi huyo alisema mataifa washirika kutosikiliza vitisho kutoka Russia, ambavyo imeyaonya mataifa ya Magharibi kutokuuvuka kile inachokiita mstari mwekundu kwenye ushirikiano wao na Ukraine katika vita vinavyoendelea.

Zelensky aidha alirudia tena ombi lake la kuruhusiwa kutumia silaha za Magharibi kushambulia ndani ya Russia.

Baada ya kikao hicho, Rais Zelensky anatarajiwa kufanya ziara nchini Italia kuzungumza na Waziri Mkuu Giorgia Meloni na kuhudhuria kongamano la uchumi.

**DW**




Gari la kubeba wagonjwa likiwa nje ya shule ya Msingi ya Hillside Endarasha, kusaidia kubeba wanafunzi walioathirika na tukio la moto. **PICHA: AP**

## Wanafunzi 17 Kenya wafa kwa moto

**NAIROBI,** KENYA

WANAFUNZI 17 wa shule ya msingi ya Hillside Endarasha wamefariki dunia baada ya bweni kuungua moto usiku wa kuamkia jana.

Wanafunzi hao wameteketea kiasi cha kutotambulika huku wengine 13 wakiwa wamelazwa hospitalini.

Hata hivyo, Rais William Ruto, ameagiza kufanyika kwa uchunguzi ili kubaini chanzo cha moto huo.

Msemaji wa polisi nchini Kenya, Resilia Onyango, alisema moto huo ulizuka kwenye bweni moja ambalo lilikuwa likitumiwa na wanafunzi 152 wa kiume.

Shughuli ya uokoaji iliendelea hadi jana jioni kwenye shule hiyo ambayo iko kaunti ya Nyeri, ambayo inapatikana eneo la kati la Kenya.

Wazazi walianza kufika shuleni hapo na maofisa wa Shirika la Msalaba Mwekundu wameweka dawati la kutoa huduma za ushauri nasaha kwa familia zilizoathirika, huku wakiwasaidia wazazi kuwatafuta na kuwatambua watoto wao.

"Tumekuja hapa kuungana nanyi na serikali kuhakikisha kwamba tumeweza kusaidiana. Tunatoa huduma ya ushauri nasaha siku ya leo na tutaendelea hadi operesheni hii hadi itakapokamilika. Tunawashukuru wananchi kwa kujitokeza haraka kusaidia." alisema kiongozi wa shirika la msalaba mwekundu, Esther Chege,

Viongozi mbalimbali wametoa rambirambi zao kufuatia tukio hilo.

Rais William Ruto aliwafariji familia zilizoathirika akilitaja tukio hilo kama la kuvunja moyo. Amewaagiza maafisa wa usalama kuchunguza na kuhakikisha wahusika wanachukuliwa hatua.

Kiongozi huyo aliahidi kuwa wizara ya usalama inafanya kila juhudi kuzisaidia familia zilizoathirika.

Naibu Rais, Rigathi Gachagua, Kiongozi wa chama cha upinzani ODM Raila Odinga, spika wa bunge la kitaifa Moses Wetangula, na mawaziri wengine pia wametuma salamu zao za rambirambi kwa familia zilizopoteza watoto wao na kuwatakia kupona harama waliojeruhiwa.

Chanzo cha moto hakijajulikana ingawa baadhi ya maofisa wanaeleza kwamba majengo mengi ya eneo hilo yamejengwa kwa mbao na sio saruji.

Bweni liloungua moto pia lilijengwa kwa mbao, na kusababisha kuwaka kwa kasi kutokana na mbao kuwa kavu.

**DW**

# MATUKIO KATIKA PICHA



Washtakiwa wa kesi ya uhujumu uchumi kwa kusafisha vipande vya meno ya Tembo 413 na meno ya Kiboko mawili yanayosadikika kuwa na thamani ya Sh. Bilioni 4.4, wakiwa chini ya ulinzi wa Askari Magereza, baada ya kusikiliza kesi inayowakabili katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**



Mfanyabiashara mdogo maarufu machinga akisaka wateja wa bidhaa zake, katika eneo la Malamba Mawili, Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe akijibu maswali yaliyoulizwa na baadhi ya Wabunge kwenye kikao cha tisa cha mkutano wa 16 wa Bunge, jijini Dodoma jana .**PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Mufti wa Tanzania, Abubakar Zuberi, akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam mapema wiki hii, wakati akitoa shukrani kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na wadau walioshiriki kufanikisha mashindano ya Kimataifa ya Quran kwa wanawake. Kulia ni Mwenyekiti wa tuzo za waliofanikisha mashindano hayo, Shekhe Othuman Kaporo. **PICHA: JUMANNE JUMA**




Mkazi wa Kata ya Kivule, jijini Dar es Salaam, Beatrice Felician, akichangia mada katika kikao cha kujadili mikakati ya kupambana na ukeketaji, kilichoitishwa na uongozi wa kata hiyo, mapema wiki hii. **PICHA: SABATO KASIKA**

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa na maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri.
Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging. Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosabisha kuwa na tundu kichwani.
Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-29

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**




"Sasa bosi ofisi yako ni ya mwisho, nimezunguka kuja kuangalia kama waliingia kwako na wameiba kitu chochote."

"Hapana, mimi hawakuchukua chochote, kila kitu kipo sawa!" Materu akaongopa. Hakutaka ijulikane kuwa amechukuliwa flashi. Labda zingekuwa za kiofisi, lakini zile ni za binafsi ambazo ni siri ambayo haikutakiwa yeyote ajue, ndiyo maana akakataa. "Sasa hawa jamaa walikuwa wanataka nini, kwa sababu wamewapiga walinzi wetu mpaka wakazimia. Halafu hawakufanya chochote wakaondoka, hawakuvunja wala nini. Nia yao ilikuwa nini?" "Labda kuna mmoja wao aligombana naye huko kwao mitaani, wakaja kulipa kisasi." Materu akaendelea kuongopa. Ni uongo ambao si halisi, lakini angalau ulimpa ahueni mzee Maliki mkuu wa ulinzi wa jengo hilo. "Wakipona mnaweza kuwauliza vizuri, wanaweza kuwa walikuja kulipa kisasi, mwenzake akataka kumsaidia kwa sababu wana silaha, wote wakaishia kupigwa."

"Ila inavyoonekana wana mafunzo ya kijeshi au ukakamavu kwa sababu hata hawa walinzi pamoja na kwamba wanajua kutumia silaha, lakini wana mafunzo maalum ya mapigano, nadhani waliwahiwa au wenzao walikuwa na mafunzo maalum. Ila nguvu yote waliyotumia imewashangaza wengi kuwa ilikuwa ni kuwapiga tu, siyo kuja kuiba chochote maana hawajachukua silaha, wala kuingia kwenye jengo ambalo lina mali, pesa na vitu vingi." Akashangaa mzee Maliki.

****************************

Alifungua droo kadhaa. Baadhi ya droo alikuta flashi lakini hazikuwa zile ambazo anahitaji. Alikuwa na 'lap top', ndogo aliyoingia nayo ambayo ilikuwa ikionyesha ni flashi ya aina gani kila anapoingiza. Aliifanya kazi hiyo kwa utulivu sana kama alivyoambiwa. Ni kwa sababu mlangoni kulikuwa na mtu ambaye alikuwa akimlinda. Hakuna hata mbu anayeweza kumsumbua, achilia mbali binadamu. Kazi hiyo ilianza saa saba ya usiku ambayo waliona ni muda uliotulia zaidi na wanaweza kufanya kazi yao kwa umakini na usahihi zaidi.

Hatimaye, alifanikiwa kupata kile ambacho alikuwa akikihitaji. Flashi ambayo aliambiwa ipo ofisini humo na ina kila kitu ambacho kitawezesha kupata ushahidi wa kile ambacho wanamtuhumu nacho.

**Pamoja na kwamba yeye hakuwa na ujuzi wa upelelezi, lakini kila alipoirudisha akili yake nyuma, akagundua kuwa hakuwa mwendawazimu wa kawaida.**

Ilikuwa ni saa nane na robo usiku. Alitumia dakika 10 kuangalia kile anachokiona anajikuta anatabasamu. "Materu umekwisha!" Akajikuta anatamka kwa sauti akiwa peke yake.

Hata hivyo bado kulikuwa na flashi mbili zilizobaki. Pamoja na kwamba aliona ushahidi umeshapatikana, lakini akaamua nazo azichomeke kwenye 'lap top'. Ya kwanza haikumvutia kwa sababu ilionekana ni ya kazi zake binafsi ambazo hazimhusu. Ya pili ilimshangaza na kumfurahisha kwa wakati mmoja. Nayo ilikuwa ni ya ushahidi wa moja kwa moja ambao unaambatana na ile ya kwanza. Akajikuta anapiga mluzi kana kwamba yupo ofisini kwake na si kama anafanya kazi moja ya hatari ambayo kama akikamatwa pale, anaweza kuuawa.

Alipomaliza akaziweka flashi zote mbili mfukoni na akarudisha zote ambazo hakuzihitaji eneo lile lile kwa uangalifu mkubwa. Ilikuwa kana kwamba hakuna kilichotokea. Hakutaka kumvutia mwenyewe mapema atakapowasili ofisini. Alitaka ajue baadaye sana kama kuna kitu kimetokea ofisini mwake. Ndiyo maana akafunga droo kwa funguo bandia alizokuwa nazo. Wala kusingekuwa na tatizo lolote kama Angetoka bila kufunga. Lakini plani haikuwa hivyo. Akazima 'lap top' yake akaweka kwenye kibegi chake kidogo. Akapiga hatua kadhaa mbele hadi mlangoni. Akaangalia ofisi kama mwenyewe akiingia kwa haraka haraka anaweza kuhisi kama kuna kitu kisicho cha kawaida. Akarejea na kukirudisha kitu vile vile kilivyokuwa mwanzo. Aliporidhika kuwa amefanya kila kitu kwa usahihi, akafungua mlango wa ofisi kwa funguo za bandia, kwa uangalifu akafunga mlango na kutembea hatua kadhaa kwa kunyata na uangaliafu mkubwa kwenda kwenye mlango mkuu.

Alipofika akamkuta mwenzake anamsubiri. Akamuuliza kwa ishara kama kila kitu kiko tayari naye akajibu kwa ishara. Wakafanya tena ishara kama wanaweza kuondoka, na wakafanya hivyo kwa haraka. Tayari ilishatimu saa tisa usiku. Walipitia kwenye kituo kikuu cha mabasi Makumbusho, wakaambaa na kukata kushoto ambako mbele walikuwa wamepaki gari lao. Wakaingia na kuondoka.

**************************************

Baada ya kupata nafuu, walinzi walisema kila kitu kilichotokea kuwa walivamiwa na watu wawili ambao hawakuwafahamu.

Wakabainisha kabisa kuwa hao watu waliwavizia na kuwapiga, huku wakibainisha walikuwa na mafunzo ya kitaalam ya mambo ya mapigano.

Wakihojiwa na polisi pamoja na waandishi wa habari, walisema baada ya kupigwa walizirai, hivyo hawakujua chochote kinachoendelea.

Hata na wao walishangaa kusikia watu wale pamoja na kufanya kazi kubwa kama hiyo, hawakuchukua chochote kile, ikiwemo hata silaha ambazo walikusanya na kuiacha pale pale.

Mmoja wa walinzi alionekana kuwa na wasiwasi na yule mwendawazimu aliyekuwa akionekana wiki tatu kabla ya tukio hilo.

Hiyo ikamshtua sana Materu. Ni kweli hata yeye alimuoa. Anakumbuka kuwa kuna siku alimuona na kuwauliza walinzi wake na wakamjibu kuwa amekuwa akipita na kwenda mara kwa mara pale na kukaa pembeni yao, lakini hana madhara na hata fujo.Pamoja na kwamba yeye hakuwa na ujuzi wa upelelezi, lakini kila alipoirudisha akili yake nyuma, akagundua kuwa hakuwa mwendawazimu wa kawaida.

"Du! Yule hakuna mwendawazimu. Yule ndiyo mpelelezi aliyekuwa anawawinda walinzi ili waingie ofisini mwangu kuchukua flasi. Hapo ndipo Materu alipogundua kuwa suala lile ni kubwa kuliko mwenyewe alivyodhani.

Ni kwamba watu walikuja na kuwapiga walinzi wa jengo lile, hawakuiba kitu chochote kile, ila walichukua flashi zake mbili ambazo zina mambo yake ya siri ambayo kama yakiwekwa hadharani, siyo tu kwamba hatogombea tena ubunge, bali hata anaweza kwenda kutundikwa kitanzini. Miguu ilimtetemeka na kujihisi kabisa yupo hatarini. Alijua kabisa kuwa flashi zile zimechukuliwa kwa sababu ya kwenda kuzitoa hadharani ili kumuumbua.

Kitu ambacho kilimtia wasiwasi zaidi ni kwamba hakujua ni lini au wakati gani ambapo watu hao watafanya kazi hiyo ya kuziweka hadharani, watatumia njia gani na mbaya zaidi hakujua ni kina nani, licha ya juhudi kubwa ya kutumia pesa nyingi kutaka kuzuia chochote kitakachoonekana kinataka kumtia doa.

Mambo yote hayo, yalimyima usingizi kabisa na kuwa na wasiwasi mkubwa licha ya utajiri alionao.

Mpaka sasa ni yeye pekee aliyekuwa anajua sababu ya watu wale kuvamia jengo hilo. Wakati wengine wakiwa na mshangao kuwa wamefanya hivyo bila kuchukua chochote, yeye anafahamu kuwa lengo lilikuwa ni kutwaa zile flashi mbili.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# SERENGETI GIRLS YATOA DOZI MICHUANO UNAF

**Na Somoe Ng'itu**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wasichana wenye umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), imeendelea kufanya vyema baada ya kuichapa Morocco mabao 5-3 katika mechi ya mashindano ya UNAF iliyochezwa jijini Tunis nchini Tunisia, juzi jioni.

Mabao ya Serengeti Girls katika mchezo huo yalifungwa na Mwatima Mwarabu na Winifrida Gerald ambao kila mmoja alipachika magoli mawili huku lingine likifungwa na Yasinta Mitoga.

> **Akizungumza baada ya mechi hiyo, Kocha Mkuu wa Serengeti Girls, Bakari Shime, aliwapongeza wachezaji wake kwa kupata ushindi wa pili mfululizo na kupata mabao tisa kwenye michezo hiyo.**

Shime alisema bado anaendelea kufanyia kazi makosa yanayojitokeza licha ya timu yake kupata ushindi.

Aliongeza anaamini kila siku wachezaji wake wanaendelea kuimarika na wataonyesha kiwango bora kwa sababu wanaendelea kuimarika.

"Sikufurahishwa namna tulivyocheza leo, hatukuwa wazuri sana hasa katika kipindi cha kwanza, hatukuwa bora, baadaye tukaamka na tupata mabao kipindi cha pili, tumeruhusu mabao mepesi sana, kikubwa na kizuri katika mpira tumefunga mabao mengi, mabao tisa ni mengi," alisema Shime.

Aliongeza siku ya juzi haikuwa nzuri kwa golikipa wake lakini ni sehemu ya kujifunza na anaamini mchezo ujao atakuja tofauti ili kuhakikisha analinda vyema lango lake.

Katika mechi ya kwanza Serengeti Girls ambayo ni timu mwalikwa katika mashindano hayo ilianza kwa ushindi mnono wa mabao 4-1 dhidi ya Misri.

Shime ameendelea kuwashukuru Watanzania waliopo Tunisia kwa kujitokeza uwanjani kuishangilia timu yao.



Mshambuliaji wa Serengeti Girls, Winifrida Gerald (kushoto), akijiandaa kumtoka mchezaji wa Morocco katika mechi ya mashindano ya Ukanda wa UNAF iliyochezwa jijini Tunis nchini Tunisia juzi jioni. Serengeti Girls ilishinda mabao 5-3. **PICHA: TFF**

# Chess yaahidi medali Olympiad

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI Vyama na Mashirikisho ya Michezo nchini vimetakiwa kuchagua wachezaji wa timu za taifa wenye viwango vya juu na si kwa ‚ukubwa' wa majina yao, timu ya Taifa ya Chess imetamba kwenda kufanya vizuri kwenye mashindano ya Olympiad.

Ofisa Michezo wa Baraza la Michezo la Taifa( BMT), Charles Maguzu, alisema hayo jana wakati akiikabidhi bendera kwa timu ya Taifa ya Chess inayotarajiwa kusafiri kuelekea Budapest, Hungary ili kushiriki michuano ya Olympiad.

"Ninatoa wito kwa vyama na mashirikisho ya michezo wachague wachezaji wa timu za taifa kwa kuwashindanisha na si kuwaingiza kwenye timu hizo kwa ukubwa wa majina yao," alisema Maguzu.

Ofisa huyo amewataka wachezaji waliopata nafasi hiyo kwenda kupambana ili kuhakikisha wanarudi nyumbani na medali za ushindi huku akiwakumbusha kudumisha nidhamu wakati wote wa mashindano.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Chess Tanzania (TACA), Geoffrey Mwanyika, alisema timu hiyo inaundwa na wachezaji 10 na kati ya hao wanawake ni watano na wanaume watano.

Mwanyika alisema hana wasiwasi na timu hiyo kwa sababu nyota wake wamechaguliwa baada ya kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali waliyoshiriki.

"Malengo yetu ni kwenda kufanya vizuri katika mashindano hayo yatakayoshirikisha nchi 193, tunaishukuru Serikali pamoja na wadhamini ambao wametusaidia kufanikisha safari yetu," alisema Mwanyika.

# Mbangula, Jeremiah, kuikabili Tabora Utd

**Na Adam Fungamwango**

MASTRAIKA tegemeo wa Prisons, Samson Mbangula na Jeremiah Juma, wamerejea kikosini kwa ajili ya kuivaa Tabora United katika mchezo wa raundi ya tatu ya Ligi Kuu Tanzania Bara utakaopigwa Septemba 14, mwaka huu kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani, Tabora.

Daktari wa timu hiyo, Damas Kinyere, alisema wachezaji hao hawakucheza michezo miwili ya mwanzo dhidi ya Pamba Jiji na Mashujaa FC kwa sababu walikuwa majeruhi, lakini kwa sasa wako fiti.

Kinyere alisema wachezaji hao wamefanya vyema mazoezi pamoja na wenzao lakini uamuzi wa mwisho ya kucheza ubakania kwa kocha mkuu.

"Wachezaji ambao hawakucheza michezo miwili ya mwanzo walikuwa watatu, tulimkosa Mbangula, Tariq Simba na Jeremiah, hawakuwa na majeraha ya kutisha sana, ni ya kawaida kwenye mpira baada ya kutibiwa tuliona wakae wapumzike, wasicheze michezo ya mwanzo wa ligi ili wapone kabisa badala ya kuwachezesha wakiwa hawajapona vizuri," alisema daktari huyo.

Naye Jeremiah, alikiri kwa sasa amepona na yuko tayari kuanza kuitumikia timu yake katika mechi ijayo.

Alisema anashukuru kwa kutocheza michezo miwili ya mwanzo na hali hiyo imemsaidia kuondoka uchovu aliokuwa nao.

"Nimecheza mechi nyingi sana, kwa hiyo kutocheza michezo miwili hii ya mwanzo kwa sababu ya majeraha nimepata muda wa kupumzika pia, kwa sasa narejea tena uwanjani kuitumikia timu yangu kwa kuifungia mabao kama kawaida," alitamba Jeremiah.

Mchezaji mwingine wa timu hiyo, Haruna Chanongo alisema licha ya kutopata ushindi katika mchezo wowote wa Ligi Kuu, wanaamini sasa wanakwenda kuvuta pointi tatu za ugenini dhidi ya Tabora United.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Shaaban Kazumba, alisema yeye na Kocha Mkuu, Mbwana Makata wamekuwa wakikomaa zaidi katika kusimamia mazoezi ya utimamu wa mwili na wanatarajia matokeo chanya kwenye mechi inayofuata.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### GALATASARAY YAMTAKA CASEMIRO

KLABU ya Galatasaray ipo katika mazungumzo na Manchester United kuhusu uhamisho wa mkopo wa mwaka mmoja kwa kiungo wao wa kati wa Brazil, Casemiro, mwenye umri wa miaka 32. (***Ali Naci Kucuk***)

### SALAH KUPEWA MKATABA

LIVERPOOL inapanga kufanya mazungumzo ya mkataba mpya na mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Misri, Mohamed Salah, mwenye umri wa miaka 32, baada yeye kusema huu unaweza kuwa msimu wake wa mwisho klabuni hapo. (***Football Insider***)

### HUERTA ALITAKIWA LIVERPOOL

KOCHA wa Pumas UNAM, Gustavo Lema, amesema Liverpool ilijaribu kumsajili winga wao wa kimataifa wa Mexico, Cesar Huerta, mwenye umri wa miaka 23. (***TUDN***}

### CHILWELL KUPELEKWA UTURUKI

KLABU ya Chelsea iko tayari kumpeleka beki wa kushoto wa England, Ben Chilwell, mwenye umri wa miaka 27 kwa mkopo nchini Uturuki, ingawa bado hawajapokea ofa yoyote. (***Telegraph***)

### FOFANA ANUKIA UGIRIKI

MAZUNGUNZO yanaendelea kati ya Chelsea na AEK Athens ya Ugiriki kuhusu uhamisho wa mshambuliaji wa Ivory Coast, David Datro Fofana, mwenye umri wa miaka 21. (***Mail***)

### CARDOSO KUTUA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur imefanya mazungumzo ya kumnunua kiungo wa kati wa Marekani, Johnny Cardoso, mwenye umri wa miaka 22 kwa dau la pauni milioni 21 kutoka Real Betis. (***Telegraph***)

### KEITA KWENDA ISTANBUL

KIUNGO wa kati wa zamani wa Liverpool, Naby Keita, mwenye umri wa miaka 29, yuko katika mazungumzo na klabu ya Istanbul Basaksehir kwa ajili ya uwezekano wa kuhamia katika klabu hiyo. (***Guardian***)

### MARTIAL MSHAHARA MNONO

WINGA wa zamani wa Manchester United, Anthony Martial, mwenye umri wa miaka 28, amepewa mkataba na AEK Athens ambao utamfanya kuwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa anayelipwa fedha nyingi zaidi klabuni hapo. (***Sport24 via Sun***)

### CABAL ATAJWA UNITED

KLABU ya Manchester United inamfuatilia kwa karibu beki wa kushoto wa Juventus mwenye umri wa miaka 23 ambaye ni raia wa Colombia, Juan Cabal. (***Tutto Juve***)

### BETIS ILIMTAKA ERIKSEN

KLABU ya Real Betis ilitoa ofa kwa kiungo wa kati wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Denmark, Christian Eriksen, mwenye umri wa miaka 32, siku ya mwisho ya dirisha la uhamisho. (***Fabrizio Romano***)

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# RONALDO AFIKISHA RASMI MABAO 900

**LISBON,** Ureno

### Mshambuliaji huyo Mreno amesema hiyo ni hatua ya kipekee...

CRISTIANO Ronaldo amekuwa mchezaji wa kwanza wa kiume kuweka historia kufunga mabao 900 katika mechi rasmi, wakati Ureno ikishinda magoli 2-1 dhidi ya Croatia kwenye mechi ya Ligi ya Mataifa ya Uefa iliyochezwa mjini Lisbon, juzi.

Ronaldo alifunga bao hilo la kihistoria kwa shuti kali la umbali wa yadi sita akimalizia krosi ya Nuno Mendes na kuifanya Ureno kuwa mbele kwa mabao 2-0 katika dakika ya 34.

**"Ina maana kubwa," alisema Ronaldo baada ya mchezo huo.**

"Ilikuwa hatua kubwa niliyotaka kufikia kwa muda mrefu. Nilijua ningefikia namba hii, kwa sababu ninapoendelea kucheza, ingetokea kawaida."

Katika sherehe hiyo, Ronaldo aliinua mikono yake usoni na kupiga magoti.

„Ilikuwa ya hisia kwa sababu ni hatua muhimu," alisema.

"Inaonekana kama hatua nyingine yoyote, lakini mimi pekee najua, na watu wanaonizunguka, jinsi ilivyo ngumu kufanya kazi kila siku, kuwa sawa kimwili na kisaikolojia, kufunga mabao 900. Ni hatua ya kipekee katika taaluma yangu."

Mshindi huyo mara tano wa tuzo ya Ballon d'Or ana mabao 58 mbele ya mpinzani wake wa karibu, Lionel Messi, mwenye mabao 842. Gwiji la Brazil Pelé anashika nafasi ya tatu kwenye orodha hiyo akiwa na mabao 765.

Ronaldo pia alikuwa wa kwanza kuvunja kizuizi cha mabao 800, akifanya hivyo mwishoni mwa 2021 akiwa katika kipindi chake cha pili akiwa na Manchester United.

Nahodha huyo wa Ureno amefunga mabao 131 ya kimataifa katika mechi 209 pia ni mabao mengi zaidi ya muda wote. Messi yuko tena wa pili nyuma ya Ronaldo kwenye orodha hiyo; yeye na mshambuliaji wa zamani wa Iran, Ali Daei wote wana mabao 109.

Pamoja na Al Nassr na United, Ronaldo pia amegawanya mabao yake 769 ya klabu kati ya Sporting CP, Real Madrid na Juventus.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 39 ameweka wazi hana nia ya kupunguza kasi wakati wowote hivi karibuni na alisema tayari analenga hatua yake ya pili ya kufunga.

"Nataka kufikisha mabao 1,000," alimwambia mchezaji mwenzake wa zamani wa United, Rio Ferdinand kwenye chaneli yake ya YouTube, akikadiria kuwa alama hiyo ya kihistoria inaweza kufikia umri wa miaka 41.

"Ikiwa sina majeraha yoyote, hii kwangu ni. jambo muhimu zaidi, nataka hilo kwangu, alama bora ninayoweza kuwa nayo katika soka ni kufikia, kwanza, mabao 900 baada ya hapo, changamoto yangu ni kuwa na mabao 1,000.

Akiwa na ushindani, Ronaldo alikuwa mwepesi kueleza ni nini kingeweka mabao yake tofauti na yale ya wafungaji wengine bora wa muda wote, wakiwemo magwiji kama vile Pelé na Alfredo Di Stéfano, ambao walicheza enzi ambazo kamera hazikuwa nyingi sana.

"Mabao yote niliyofunga, yana video," alisema. „Wote wana video. Sikiliza, ninawaheshimu wote Pelé na Di Stéfano. Na kama unataka mabao zaidi, ninaweza kuwaleta kutoka mazoezini pia. Na nitathibitisha kwa watu baadaye. Wanampendelea mchezaji huyu, au hii ndiyo bora zaidi sijali kuhusu hilo.

## HABARI MICHEZO

# CASEMIRO AKATAA KUTUA GALATASARAY




**MANCHESTER,** England

CASEMIRO amedhamiria kupigania mustakabali wake ndani ya Manchester United na anapanga kukataa mapendekezo yoyote kutoka kwa wababe wa Uturuki Galatasaray katika siku zijazo, ripoti imefichua.

Kiungo huyo mkongwe alikabiliwa na mzozo msimu uliopita kwa kucheza vibaya mfululizo na kujikuta akikabiliwa na shutuma nyingi kufuatia United kuchapwa mabao 3-0 na Liverpool, ambapo alitolewa kipindi cha mapumziko baada ya kufanya makosa mawili na kusababisha mabao.

Ripoti kutoka Uturuki, ambazo baadaye ziliungwa mkono na gazeti la The Times, zilidai Galatasaray walikuwa wakipanga kumnunua Casemiro kabla ya dirisha lao la uhamisho kufungwa Septemba 13, mwaka huu.

Hata hivyo, Daily Mail imeripoti Casemiro hana nia ya kuondoka United.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, ambaye ana mataji matano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Real Madrid, anataka kujenga upya heshima yake na kujidhihirisha Old Trafford kwa mara nyingine.

Inaaminika United wako tayari kutoa ofa kwa Casemiro, ambaye bado ana miezi 18 kwenye mkataba wake unaomfanya alipwe pauni 375,000 kwa wiki ambao pia unajumuisha chaguo la kuongezewa mwaka mmoja, lakini Mashetani Wekundu bado hawajapokea nia yoyote madhubuti.

Presha iko kwenye mabega ya Casemiro baada ya kuondolewa katika kikosi cha Brazil kwa ajili ya michuano ya Copa America majira ya kiangazi.

Kocha, Dorival Junior hajamwita kiungo huyo kwa mechi za kimataifa za Septemba.

Katika ngazi ya klabu, United walitumia fedha nyingi kumnunua Manuel Ugarte kutoka Paris Saint-Germain mwishoni mwa dirisha la majira ya joto.

Kiungo huyo mkabaji mwenye umri wa miaka 23 ni wazi ndiye atakayechukua nafasi ya Casemiro kwa muda mrefu na ataongeza ushindani kwa dakika msimu huu.

## Newcastle haihofii kuondoka Howe

**NEWCASTLE,** England

MKURUGENZI wa Michezo wa Newcastle United, Paul Mitchell, amekiri haogopi uvumi kuhusu Kocha, Eddie Howe, huenda akamrithi Gareth Southgate kwenye kikosi cha England.

Bosi huyo wa Magpies kwa muda mrefu amekuwa akihusishwa na kibarua cha England, kwanza wakati Roy Hodgson alipomaliza mwaka wa 2016, na tena sasa baada ya kuondoka kwa Southgate.

Ingawa mbadala wake wa kudumu bado haujapatikana, kocha wa timu ya taifa ya England ya Vijana chini ya miaka 21 Lee Carsley ameteuliwa kuwa kocha wa muda kwa mechi zijazo za Ligi ya Mataifa dhidi ya Jamhuri ya Ireland na Finland.

„Tunamtaka Eddie Howe awe kocha wetu mkuu kwa muda tuwezavyo lakini pia tunatambua tuko safarini,“ alisema akiwaambia waandishi wa Habari.

"Pia tunatambua ubora wake na uwezo wake pia. Sijawahi kuwa mtu wa kuogopa kupendezwa na wafanyakazi wetu, haswa kocha mkuu, na haswa kutoka ngazi ya shirika ambayo FA.

„Kama Mwingereza, ninajivunia, na nadhani ni utambuzi wa miaka miwili na nusu ambayo amekuwa hapa na kazi aliyoifanya Bournemouth. Ni mtaalamu mzuri sana anayetambuliwa kwa kile alichokifanya.“





# Chelsea yamtema Palmer Uefa

**LONDON,** England

CHELSEA imefanya uamuzi wa kushtukiza wa kumwacha nyota wao, Cole Palmer kwenye kikosi chao cha Ligi ya Europa Conference.

Palmer amekuwa na mafanikio zaidi kuliko usajili mwingine wowote ambao The Blues wamefanya katika miaka miwili iliyopita, akifunga mabao 25 baada ya uhamisho wake kutoka Manchester City.

Lakini jina lake halikuwepo wakati Chelsea ilipochapisha maelezo ya kikosi cha wachezaji 25 kilichochaguliwa kwa ajili ya mashindano ya hayo ya Europa - ambayo sasa yamesimama hadi Februari, ambapo hadi mabadiliko matatu yanaweza kufanywa.

The Blues pia walichagua kuwaacha Wesley Fofana na Romeo Lavia kwa sasa.

Palmer ana umri wa miezi michache sana na pia hajakaa Chelsea kwa muda wa kutosha.

Fofana pia amekuwa muda mrefu hapo wakati Lavia amekuwa tu na klabu hiyo tangu msimu wa joto uliopita badala ya miaka miwili inayohitajika ili kustahili.

Orodha ya wachezaji 25

Makipa: Robert Sanchez, Filip Jorgensen, Lucas Bergstrom huku mabeki ni Axel Disasi, Marc Cucurella, Tosin Adarabioyo, Benoit Badiashile, Reece James, Malo Gusto, Renato Veiga.

Viungo: Enzo Fernandez, Noni Madueke, Carney Chukwuemeka, Kiernan Dewsbury-Hall, Moises Caicedo, Cesare Casadei na safu ya washambuliaji itakuwa na Pedro Neto, Mykhailo Mudryk, Joao Felix, Nicolas Jackson, Christopher Nkunku, Jadon Sancho, Marc Guiu.

HABARI MICHEZO

## Yanga: Tutawamaliza..

INATOKA UKURASA 24

Yanga yalifungwa na Shekhan Ibrahim, Salum Aboubakar 'Sure Boy' na Mkongomani Jean Baleke.

Yanga imesonga mbele katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa kuifunga Vital'O ya Burundi jumla ya mabao 10-0, katika mechi mbili ambazo zote zilichezwa, Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Awali iliichapa mabao 4-0, kabla ya kuikandika magoli 6-0 katika mchezo wa mkondo wa pili, ambapo wapinzani wao waliamua kuuchagua Uwanja wa Azam kutokana na viwanja nchini kwao kutokidhi vigezo vya Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF).

## Simba SC..

INATOKA UKURASA 24

"Ikikamilika Ubaya Ubwela, iko full pakti, ni mateso, hii Simba sio ya kawaida, hii Simba tumewekeza, na mwaka huu tumedhamiria Ubaya Ubwela," Ahmed alisema.

Aliongeza wanawaomba radhi mashabiki wao kwa kutoruhusu watazamaji katika mechi ya leo ambayo inachezwa ndani ya Kalenda ya FIFA.

Alimtaja mchezaji ambaye ni majeruhi katika kikosi chao ni golikipa, Ayoub Lakred huku akiongeza kiungo mshambuliaji, Fabrice Ngoma, amerudi kikosini baada kurudi nchini akitokea nyumbani kwao Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, kutokana na matatizo ya kifamilia.

"Mchezo huo utachezwa milango ikiwa imefungwa, kwa sasa mechi ambazo zinatakiwa kuwa na mashabiki ni zile zilizoko katika Kalenda ya FIFA tu, kwa hiyo mashabiki wetu waelewe hilo," Ahmed alisema.

Aliongeza katika mechi hiyo kocha anataka kuona wachezaji wake wakicheza bila presha yoyote na ndio sababu ya kuamua kujipima dhidi ya Maafande hao wa JKT Tanzania.

Simba inatarajia kutumia mechi hiyo ya pili ya kirafiki kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wa raundi ya kwanza ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Al Ahly Tripoli, utakachezwa ugenini Septemba 15, mwaka huu na marudiano yakitarajiwa kufanyika hapa nchini baada ya wiki moja.

# COASTAL UNION YAISHUKURU SIMBA SC KUWAACHIA LAWI

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya sintofahamu ya muda mrefu kuhusiana na usajili wa mchezaji, Lameck Lawi, imeamuliwa nyota huyo ataitumikia timu yake ya zamani, Coastal Union, imefahamika.

Lawi ambaye alikuwa anagombewa na Simba na Coastal Union, sasa ataonekana uwanjani Septemba 13, mwaka huu wakati Wagosi wa Kaya watakapoivaa Mashujaa FC.

Ofisa Habari wa Coastal Union, Abbas El Sabri, amesema baada ya mazungumzo na Simba, hatimaye wamefikia mwafaka wa mchezaji huyo kusalia kwao, hivyo tayari wamefunga rasmi sakata hilo.

"Suala la Lawi limekuwa na maswali mengi sana, lakini majibu yake yatapatikana Septemba 13, mwaka huu tutakapomtumia katika mchezo wetu dhidi ya Mashujaa FC, hapo tutakuwa tumejibu kila kitu tulichoulizwa, hili jambo limeshamalizika, huyu kwa sasa ni mchezaji halali wa Coastal Union," alisema El Sabri.

Aliongeza walikaa vikao viwili baada ya Kamati ya Sheria na Hadhi ya Wachezaji kuwataka kumalizana wenyewe na hatimaye wamefikia makubaliano mazuri.

"Ni kweli Simba wamekuwa waungwana, tumekaa nao vikao viwili na tumekubaliana, uungwana ndiyo unaotakiwa kwenye mpira, nasi pia tunawashukuru wenzetu, sisi pia tunaahidi tutafanya uungwana zaidi kwao, tunawashukuru sana," aliongeza.

Wakati huo huo, Coastal Union, inatajwa huenda ikamchukua Kocha Mrundi Dominique Niyonzima, kwa ajili ya kurithi mikoba ya David Ouma, aliyetimuliwa.

El Sabri alikiri kuwa wapo katika mchakato wa mwisho kumtangaza kocha, lakini hatutakataa wala kukubali kumtwaa kocha huyo.

"Mpaka sasa tunakamilisha mchakato wa benchi la ufundi, ambalo tunaamini litatuvusha. Tumesikia tunahusishwa na Kocha Niyonzima, na sisi tunafurahi kwa sababu tunahusishwa na mmoja na makocha wakubwa kabisa katika ukanda wetu wa Afrika Mashariki na Kati, sisi pia tuna ndoto ya kuwa na kocha kama huyo," aliongeza.



Wachezaji wa Simba Queens wakifanya mazoezi ya ufukweni kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya Ngao ya Jamii kwa Wanawake yanayotarajiwa kufanyika kuanzia Septemba 24 hadi 27, mwaka huu kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA SC**

# Mabao 22 Ligi Kuu yachambuliwa

**Na Adam Fungamwango**

MABAO 22 yamefungwa katika michezo 13 ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa mpaka sasa, 19 yakifungwa kwa njia ya kawaida na matatu kwa mikwaju ya penalti.

Kwa mujibu dawati la takwimu la michezo la gazeti hili, jumla ya mabao 18 yamefungwa ndani ya eneo la hatari na manne yamefungwa nje ya boksi.

Takwimu zinaonyesha mabao hayo yamegawanyika sehemu tatu, ambapo 14 yamefungwa kwa mguu wa kulia na wachezaji wa timu mbalimbali za ligi hiyo, matatu yamefungwa kwa mguu wa kushoto na matano yamefungwa kwa vichwa.

Mabao matatu ya mguu wa kushoto yamefungwa na Joshua Ibrahim wa KenGold huku Valentino Mashaka wa Simba akifunga, Agosti 17 wakati timu hiyo iliposhinda mabao 3-0 dhidi ya Tabora United na Heritier Makambo wa Tabora United, akifunga kwa penalti dhidi ya Namungo.

Takwimu pia zinaonyesha mabao 14 tu yamefungwa katika mechi za raundi ya kwanza msimu huu iliyokuwa na michezo minane, ikiwa ni machache kuliko yaliyofungwa raundi hiyo msimu uliopita ambapo jumla ya mabao 22 yalifungwa.

Msimu uliopita, Ligi Kuu Tanzania Bara ilianza kwa Geita Gold kushinda bao 1-0 dhidi ya Ihefu, JKT Tanzania kuichapa Namungo bao 1-0, Dodoma Jiji ikaichapa Coastal Union mabao 2-1, Mashujaa ikashinda mabao 2-1 dhidi ya Kagera Sugar, Azam ikaibabua Tabora United mabao 4-0, Simba ikashinda mabao 3-2 dhidi ya Mtibwa Sugar, Singida Fountain Gate na Prisons zikatoka suluhu na Yanga ikapata ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya KMC.

Michezo
Nipashe
Jumamosi Septemba 7, 2024



Ronaldo afikisha rasmi mabao 900

UKURASA 21



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa Afrika (AFCON 2025), dhidi ya Guinea itakayochezwa ugenini Septemba 10, mwaka huu. **PICHA: TFF**

# Simba SC yatamba kutembeza vichapo

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI inatarajia kushuka dimbani leo kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya JKT Tanzania, uongozi wa Simba umesema hawatarudia makosa yaliyojitokeza misimu mitatu iliyopita.

Simba imeshindwa kutwaa taji la Ligi Kuu Tanzania Bara ambalo kwa misimu mitatu mfululizo limechukuliwa na wapinzani wao Yanga.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema kikosi chao kinaendelea kuimarika, hivyo wanatarajia kupata matokeo mazuri katika kila mechi watakayocheza.

Ahmed alisema wanatarajia watawapa furaha mashabiki wao kwa kufanya vyema katika mashindano yote watakayoshiriki na hii inatokana na usajili mzuri uliofanywa.

INAENDELEA UK. 23

# Yanga : Tutawamaliza CBE kwao

## ●●● Gamondi asema hii itawaweka salama kabla ya marudiano kwa sababu...

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kubakia na wachezaji wachache kambini, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, ameendelea na programu yake kwa ajili ya kujiandaa kuwakabili CBE ya Ethiopia katika mchezo wa raundi ya kwanza ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

CBE watawakaribisha mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga Septemba 14, mwaka huu kwenye Uwanja wa Abebe Bikila ulioko jijini Addis huku mechi ya marudiano ikitarajiwa kufanyika wiki moja baadaye kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Hata hivyo Gamondi ameanza mazoezi akiwa na wachezaji 11 tu kutokana na nyota wengine kuitwa katika majukumu ya kimataifa.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, aliliambia gazeti hili Gamondi anaendelea na programu yake kwa sababu anataka wachezaji waliobakia pia kuwa fiti na tayari kwa mchezo huo wa ugenini.

**Alisema wanafahamu mchezo huo hautakuwa rahisi na ndio sababu wameanza mapema mazoezi kwa sababu wanataka kwenda kuvuna matokeo mazuri ugenini.**

"Yanga imesajili wachezaji 27, kati ya hao 14 wamekwenda kuziwakilisha nchi zao katika michezo wa kimataifa, wengine wameitwa Taifa Stars, Mali, Burkina Faso, Zambia, Kenya, Uganda na kwingine, tumebakiwa kambini na wachezaji 13 tu na kati ya hao wawili wana majeraha," alisema Kamwe.

Aliongeza pia katika kikosi chao wana wachezaji wawili majeruhi ambao ni Yao Kouassi na Farid Mussa.

"Kwa maana hiyo tumebakiwa na wachezaji 11 tu, lakini mwalimu bado anaendelea na programu yake kama kawaida, amehitaji mchezo mmoja wa kirafiki ili kujipima na kuangalia utimamu wa mwili wa wachezaji wake, anajua wale wengine watarudi wakiwa fiti kwa sababu wanaenda kuzipambania nchi kwa kucheza mechi ngumu," Kamwe alisema.

Aliongeza anakiandaa kikosi chake kuonyesha kiwango kizuri katika mchezo huo na tayari wameshaanza ‚kuwasoma' wapinzani wao.

"Gamondi alihitaji mchezo wa kirafiki na sisi tukaamua kuwaita wenzetu wa Kiluvya FC tukacheza nao, ilikuwa ni mechi ya kirafiki na ya kimazoezi, haikuwa na shabiki yoyote aliyeruhusiwa kuingia kutazama kwa sababu tulikuwa tumebakiwa na wachezaji 11, tukalazimika kuwaongeza wachezaji watatu wa kikosi cha pili.

Kwa bahati nzuri ulikuwa mchezo mzuri, haukuwa wa kukamiana, tukashinda mabao 3-0, na tunafikiria siku hizi chache zingine tucheze mechi nyingine kama hii, ambapo mwalimu amehitaji tena ili kuwaimarisha nyota wake walioko kabla wale wengine hawajarejea nchini," aliongeza ofisa huyo.

Alisema maandalizi ya safari ya kuelekea Ethiopia yako katika hatua za mwisho na wanaamini wakiwa ugenini wataendeleza ‚moto' waliounza katika mashindano hayo ya kimataifa msimu huu.

Mechi dhidi ya Kiluvya FC ilichezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex na mabao ya

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >